# Uislamu
# Na Dini Nyingine

Na

Hadhrat Mirza Bashir-ur-Din Mahmood Ahmad[ra]
Khalifatul-Masih II

**Uislamu Na Dini Nyingine**

Islam Aur Deegar Mazaahib (Swahili Translation)

Tafsiri ya Kiswahili ya:
Islam Aur Digar Madhaahib (Kiurdu)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Bashir-ur-Din Mahmood Ahmad[ra]
Khalifatul-Masih II

**Mfasiri:**
Jamil R. Rafiq

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1916
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 1967
Chapa ya pili (Kiswahili): 2020

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**
**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover designed by: Usman Nasir Choudhary

ISBN: 978-1-84880-526-2
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# NENO LA MBELE

Makala hii iliandikwa, kwa lugha ya Kiurdu, na Seyidna Amirul Muminin, Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmood Ahmad (1889-1965), Khalifa wa Pili wa Seyidna Ahmad$^{as}$, Mungu awe radhi naye, nayo ilisomwa katika mkutano wa watu wote uliofanyika mjini Delhi, India tarehe 6, mwezi Machi, mwaka 1916.

Kwa kuwa ni makala nzuri sana ielezayo ukweli wa dini ya Kiislamu na ukamilifu wake, Hadhrat Amirul Muminin Hafidh Mirza Nasir Ahmad, Khalifa wa Tatu wa Seyidna Ahmad$^{as}$, Mungu amsaidie, aliniamrisha kuifasiri kwa Kiswahili ili wajuao lugha hii pia wafaidika kwayo. Namtolea Mwenyezi Mungu shukurani aliyeniwezesha kutekeleza amri hii ya Khalifa wake Mtukufu.

Vilevile sina budi kumshukuru mheshimiwa Maulana Sheikh Muhammad Munawwar, Mbashir Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya nchini Tanzania, ambaye juu ya kuwa na kazi zake nyingi alisoma kwa uangalifu tafisiri hii kwa kuisahihisha kabla ya kupiga chapa.

Wasalaam,
Jamil-ur-Rahman Rafiq, B.Sc.
9 Machi 1967

نَحْمَدُهُ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ[2] بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[1]

# UISLAMU NA DINI NYINGINE

Kabla sijaanza kueleza madhumuini ambayo wakati huu nimesimama kutaka kuyaeleza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia nguvu ambazo kwa sababu yake tukaweza kufikiria mambo yaliyo magumu kufahamika yanayotuwezesha kuifikia Dhati iliyo nyuma ya mapazia mengi ambayo ni Mwumba, Mwenye kuruzuku na Mmiliki wa viumbe vyote vipatikanavyo. Naam, ninamshukuru yule Mfalme ambaye juu ya kuwa na uwezo usiokadirika na kudrua zake zisizo na mipaka, na juu ya utakatifu wake mwingi, akaelekea kumwongoza mwanadamu aliye mnyonge na dhaifu na akampa uwezo na elimu ambazo kwazo binadamu anaweza kufika barazani mwa Bwana wake na kumkaribia yeye kwa kuviondolea mbali vizuizi vyote vya njiani na kuyararulia mbali mapazia yote. Tena ninamshukuru mara ya tatu yule Mfalme ambaye kwa kuona udhaifu wa binadamu akawateua kwa fadhili na hisani zake, watu watakatifu na watawa miongoni mwa wanadamu ili wasikie maneno yake mtatamu na waweke msingi wa imani yao juu ya mwamba madhubuti wa kuona hasa, na ambaye akawapa hao ishara zenye nguvu

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingiwa Rehema na Ukarimu.
[2] Twamhimidi Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

ambazo kwa kuziona hizo watu wengine wenye shauku ya kufuata ukweli wakamilishe imani yao. Namshukuru tena Mola Wangu Mwenye hisani aliyetupa serikali ambayo chini ya utawala wake wa amani tunaweza kupeana mawazo juu ya mambo ya dini, na kuwafikishia ndugu wengine matokeo ya upelelezi wetu bila ya hofu wala hatari yoyote.

## Uislamu Unasadikisha Manabii wote wa Dunia

Baada ya hayo, napenda kuelekeza fikira zenu kwenye jambo hili ya kwamba si kusudio langu wakati huu kulinganisha Uislamu na dini zingine kwa njia ya kuzivurumishia masingizio kadha dini hizo na kusema kuwa hizo zote ni za uwongo na ya kwamba dini ya Kiislamu tu ndiyo dini iliyoletwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwaongoza wanadamu. Kwa maana, nikifanya hivyo siyo kwamba akili tu ya binadamu itakataa fikira yangu hii kwa nguvu sana, bali Uislamu pia utajiweka kando nayo. Kwa sababu, Uislamu haukiri kuwa Mwenyezi Mungu ni dhalimu, wala hautaki kuikubalisha dunia kwamba Mtume[saw] alipokuwa hajafika duniani, Mwenyezi Mungu alikuwa hajaumba njia yoyote kumwongoza mwanadamu. Ikiwa Mwenyezi Mungu ameendelea tangu kale kuwatimizia wanadamu mahitaji yao ya kimwili, basi kuna sababu gani ya kutokuwatimizia mahitaji yao ya kiroho na kuwaacha upotevuni kwa miaka malaki na malaki? Uislamu unapinga vikali fikira kama hiyo na unamkiri Mwenyezi

Mungu kuwa Mola wa walimwengu wote; yaani ulezi wake unahusu kila zama na kila nchi, wala hauihusu kaumu fulani tu au zama fulani. Kama vile jua lake lilivyoendelea siku zote kuwaangazia wanadamu kimwili, ndivyo hivyo nuru yake ya kirho ilivyoenelea kuangazia tangu kale akili ya binadamu kwa miali yake ing'aayo. Na kama maji yaliyo matengenezo ya hewa za namna kadha yalivyoendela kuteremka kutoka kwake ili kuurutubisha mwili wa kibinadamu, ndivyo hivyo wahyi wake ulivyo matengenezo ya usawa na ukweli ulivyoendelea kushuka kutoka kwake ili kuirutubisha roho. Yeye hakuinyima kaumu yoyote hisani zake. Hakuwafanyia ubahili wenyeji wa Bara Hindi wala wenyeji wa Uajemi. Hakuwazuilia Wachina kipawa chake wala Waarabu. Mvua yake ya kiroho haikukataliwa isiinyeshee Asia au Ulaya; misitu ya Amerika haikunyimwa wala majangwa ya Afrika. Kurani Tukufu yatangaza kwa nguvu sana:

وَإِنْ مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ

"Na hakuna taifa lolote ila alipita humo Mwonyaji", (35:25)

Kadhalika yasema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ۖ

"Na bila shaka Tulimwinua mtume katika kila umati ya kwamba Mwabuduni Mwenyezi Mungu na mwepukeni Mwovu", (16:37)

Isitoshe, Mtume wetu[saw] alisema ya kwamba katika India pia baadhi ya mitume wamepita. Na alipoulizwa kuhusu Uajemi alisema: ndiyo, lugha ya Kiajemi pia haikunyimwa maneno ya Mungu, na ufunuo wake uliendela kushuka katika lugha hiyo vilevile.

Basi katika hali kama hii niliganishapo Uislamu na dini zingine, siwezi kushika kani na kusema dini iliyoshika kuiongoza dunia ndiyo ile tu iliyomteremkia Mtume[saw]. madai kama hayo yatakuwa kinyume tu cha Uislamu. Wakati wa kulinganisha dini mbalimbali, hali yangu ni mbali kabisa na hali ya wafuasi wa dini nyingine zote; maana, hao hushurutishwa kuwakadhibisha manabii wa mataifa mengine ili kuhakikisha ukweli wa manabii wao. Lakini mimi nalazimika kuwasadikisha manabii wa dunia nzima kwa kuthibitisha ukweli wa yule Nabii[saw] ambaye nina fahari kuwa mtumwa wake. Mwaria[3] huona madai ya Marishii,[4] wlioleta Maveda,[5] yako salama mpaka hapo tu asipothibitika mpendwa yeyote wa Mungu na mtawa mwenye kupata ufunuo moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Basi, yeye huwakadhibisha wakweli wote waliotumwa katika nchi mbalimbali kwa kuwaongoza bindamu, ili kuhakikisha ukweli wa dini yake. Myahudi au Mkristo huona

[3] Aria ni madhehebu katika dini ya Kibaniani.
[4] Marishii ni Watawa wa dini ya Kibaniani.
[5] Maveda ni vitabu vya dini ya Kibaniani.

heshima ya vitabu vyote vingine vilivyoteremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwaongoza wanadamu walioishi katika nchi ghairi ya Sham, vikadhibishwe; basi yeye hubatilisha kabisa dini zingine kwa kuisaidia dini yake. Kadhalika mfuasi wa dini ya Zorosta aona hasara kubwa kwa dini yake katika kitabu kufunuliwa nje ya nchi ya Uajemi; hivyo hukadhibisha manabii wote waliofika katika nchi zisizokuwa Uajemi, na kufikiria vitabu vyote na wahyi wote ulioteremka nje ya Uajemi kuwa uzushi wa wanadamu.

Kwa kifupi, wafuasi wa dini zote, isipokuwa Islam, wajuapo matokeo ya upelelezi wa wagunduzi wa historia ya kale, kwamba katika zama fulani, mtu fulani alidai utume katika nchi nyingine, au kitabu kingine kilisimuliwa kuteremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi hushtuka mara moja kwamba adui mwingine tena wa dini yao amezalika. Lakini kinyume na hayo, hali ya Mwislamu ni kwamba anapotajwa mbele yake nabii yeyote wa nchi yoyote, moyo wake huruka kwa furaha, kwani hupata dalili nyingine ya ukweli wa Kurani Tukufu, na maneno haya yaliyojaa ukweli yaja mbele ya macho yake, ya kwabma:

وَإِن مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ

"Na hakuna taifa lolote ila alipita humo Mwonyaji", (35:25)

Kadri hesabu ya manabii na vitabu ithibitikavyo katika nchi mbalimbali, ndivyo yathibitikavyo zaidi madai ya Kurani Tukufu kwamba manabii wamepita katika kila taifa. Na zaidi ya Uislamu dini nyingine zithibitike hata ngapi, Mwislamu nafurahika kwa kuzijua badala ya kuhuzunika.

Basi, wakati wa kulinganisha Uislamu na dini zingine, si kazi yangu nithibitishe kwamba dini nyingine zimebuniwa tu na watu, na ya kuwa Manabii na Marishii wa mataifa mengine — Mungu apishe mbali — walikuwa waongo. Bali ni faradhi yangu, nikiwa Mwislamu, kuwasadikisha wakweli wote waliopita katika mataifa na nchi mbalimbali. Kama ninavyosadikisha manabii wa Wana wa Israeli, inanipasa nikiri bila kusita ukweli wa watawa waliopita katika Bara Hindi, Ram na Karishna, na kukubali ukweli wa Zorosta, mtawa wa Uajemi. Na mkweli yeyote wa taifa lolote aliyedai kuwa ametumwa na Mungu kisha alipata msaada na nusura kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu aliwafanya watu kwamba wamkubali, ni faradhi yangu kumkubali kuwa alitoka kwa Mwenyezi Mungu. Maana, Kurani Tukufu inaniambia:

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اَوْ كَذَّبَ بِاٰيٰتِهٖ ؕ اِنَّهٗ لَا يُفْلِحُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿۲۱﴾

> "Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye uwongo Mwenyezi Mungu au

azikadhibishaye ishara zake? Hakika wadhalimu hawatafaulu," (6:22).

Na ikiwka mtu kama huyo pia aweza kufanikiwa katika kusudio lake, basi, tena, kuna tofauti gani kati ya watokao kwa Mwenyezi Mungu na waongo?

## Haja ya Uislamu hali Dini zingine zipo!

Sasa, lajitokeza swali kwamba ikiwa Uislamu unasadikisha dini zingine zote zilizopatikana na kuenea katika nchi mbalimbali kwamba zimetoka kwa Mungu, basi, tena, kuna haja gani ya Uislamu ilhali dini hizo zipo? Na kuna faida gani ya kuhubiri Islam kwa wafuasi wa dini zingine zilizopo?

Basi, jibu lake ni hili. Islam inakiri ya kuwa hii si dini ya kwanza, bali kabla yake vilevile Mwenyezi Mungu aliendelea kuwatuma Mitume ili kuwongoza watu wa kila taifa. Papo hapo yadai kwamba dini zote zilizofika kabla ya Uislamu zilifaa kwa mahitaji machache ya zama zile tu. Kwa hiyo manabii mablimbali walikuwa wanatumwa kwa kila taifa ili wanadamu watayarishwe kwa maendeleo ya juu sana yaliyokadiriwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili yao. Katika zama za Mtume[saw], kwa sababu ya umbali mwingi kutoka zama za manabii, dini zote zilikuwa zimefika ukingoni mwa maangamio. Na binadamu, kwa kuongeza mambo mengi, kwa sababu ya upumbavu wake, katika elimu halisi zilizoletwa na

Mwenyezi Mungu, alikuwa amechafua chemchemi hii safi, kama asemavyo Mwenyzi Mungu:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُمْ بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٤٢﴾

> "Ufisadi umedhihirika barani na baharini kwa sababu ya yale iliyoyafanya mikono ya watu, ili Awaonjeshe (adhabu ya) sehemu ya waliyoyafanya huenda warudie", (30:42).

Muradi wa 'Bara' ndani ya Kurani Tukufu humaanisha Akili Tupu isiyosaidiwa na wahyi wa Mungu; na 'Bahari', muradi wake ni Neno la Mungu. Basi, maana ya aya hii ni kwamba wakati huu matokeo ya maovu ya watu yamedhihirika kwa njia ya kuwa upande mmoja tamaa za nafsi zimetia pazia juu ya akili za watu, na akili za watu zaendelea kuchafuka kwa sababu ya wingi wa matamanio mabaya. Na mataifa yategemeayo akili tupu, yaendelea kujinyima kufikia hata lile daraja ambalo kwalo akili tupu yaweza kumfikisha binadamu. Na upande mwingine Neno la Mungu pia limeharibika. Ndio kusema kuwa watu wameishalichafua kwa kuongeza fikira zao ndani ya Neno lililowashukia manabii waliotumwa na Mwenyezi Mungu katika nchi na zama mbalimbali ili kuwaongoza wanadamu. Hivyo, yale mataifa ambayo yalikuwa yametegemea Neno la Mungu nayo yalikuwa yakinywa katika chemchem hii safi, sasa, kwa sababu ya chemchem hii kuchafuliwa, hayawezi kujipatia faida

za kiroho zilizokuwa zinapatikana zamani katika maji haya safi. Kwa hiyo, kati yao vilevile maovu yanaendela kuenea pamoja na udhaifu.

Basi, hali ya dunia ilipokuwa hivi, ilibidi kwamba Mwenyezi Mungu Aliye Mwingi wa huruma kwa watu wake awaangalie na kuwaokoa katika maangamio.

Kwa hakika, katika zama za Mtume[saw] hali ya wafuasi wa dini mbalimbali ilikuwa kama watu walioshika kamba zilizoning'inia kutoka juu ya mnara mrefu wakitaka kupanda mnarani lakini walipofika ukingoni mikono yao ikalegea na kuachana nazo. Hakuna cha kuwazuia wasianguke chini isipokuwa tu kwamba nguo zao zikajizinga na sehemu fulani ya kamba, basi wakabaki kuning'inia kichwa chini hewani.

Katika nyakati mbalimbali manabii walianza kuyapandisha mataifa mbalimbali juu ya mnara mrefu wa kiroho, na kwa ajili hiyo, bila shaka nguvu za kirho zikapata maendeleo. Lakini katika zama za Mtume[saw], kwa sababu ya umbali mwingi kutoka zama za manabii, wafuasi wa dini mbalimbali walikuwa wamerudi nyuma kwa vitendo na itikadi. Kama hangefika, wakati huo, mwenye kuwaita kwenye mwongozo, wangeangamia kabisa na juhudi zote walizofanya manabii mbalimbali zingepotea bure. Lakini, kama Kurani idaivyo, huyu Mwokozi wa dunia akaja katika wakati hasa. Naye kwa kuwashika shika akawapandisha juu wale watu

waliokuwa wamening'inia kichwa chini, ambao japo walikuwa wamekwisha fika karibu na kilele cha mnara lakini katika hali yao hiyo walikuwa hatarini zaidi kuliko waliosimana chini. Na wale waliokuwa wakijaribu kupanda kutoka pande mbalimbali, Mtume[saw] akawakusanya mahali pamoja juu ya mnara. Na ikawekwa dini moja na kitabu kimoja tu, kwani maendeleo ya utamaduni yalikuwa yamefanya dunia nzima kama nchi moja, na wanadamu wote kama taifa moja. Na hiyo ilikuwa ni siku ya kwanza ulipofuatwa 'Udugu wa Binadamu' kikwelikweli, na Mtume[saw] akatangaza kwa sauti kuu kwa mujibu wa amri ya Mwenyezi Mungu ya kwamba:

قُلْ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنِّى رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا ٱلَّذِى لَهُۥ مُلْكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۖ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ يُحْىِۦ وَيُمِيتُ ۖ
فَـَٔامِنُوا۟ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِ ٱلنَّبِىِّ ٱلْأُمِّىِّ ٱلَّذِى يُؤْمِنُ بِٱللَّهِ وَكَلِمَٰتِهِۦ وَٱتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥٩﴾

> 'Enyi watu, hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyote Ambaye Anao ufalme wa mbingu na ardhi, hapana aabudiwaye ila Yeye, Ahuishaye, Afishaye. Basi Mwaminini Mungu na Mtume wake, aliye Nabii Ummi, ambaye humwamnini Mwenyezi Mungu na maneno yake, na mfuateni yeye ili mpate kuongoka'. (7:159)

Katika aya hii Mwenyezi Mungu ameashiria ya kwamba Mtume mmoja tu ametumwa kwa dunia nzima ili kwamba kwa njia hii Mwenyezi Mungu, aliye Mungu Mmoja tu wa ardhi na mbingu, ajidhihirishe katika dunia

nzima kwa utukufu wake wote kwa njia ya Mtume mmoja tu, na Umoja wake uonekane kwa njia mpya. Na iliwezekanaje ya kuwa angeacha dunia hivi hivi tu, wakati huo, hali yu Mwenye kuhuisha na kufisha? Basi sifa yake ya kuhuisha ilitaka kuihuisha tena ardhi iliyokuwa imekufa. Na zile dini ambazo hazikufaa kwa kuiongoza dunia, zihesabiwe pamoja na dini zilizokufa. Yaani baada ya kuzifuta dini hizo aeneze duniani ile dini ifaayo na itimizayo mahitaji yote ya binadamu. Na madai kama haya hawakuyafanya Marishii wa Bara Hindi wala Mwenye busara wa Uajemi wala manabii wa Sham; bali hao walikuja kwa taifa moja au nchi moja tu. Na ikiwa taifa lolote lilipanua mahubiri yake wakati fulani, basi hayo ni kinyume cha maagizo ya waanzilishi wa dini hizo baada ya wao kufariki. Kama ithibitikavyo katika historia ya dini kubwa miongoni mwa dini zinazohubiriwa, ghairi ya Uislamu — yaani dini ya Kikristo — ya kwamba Yesu alikataza isihubiriwe kwa wote, lakini baada yake ilianza kuhubiriwa kwa watu wote. Basi hayawezi mahubiri hayo kuitwa ni sehemu ya dini hiyo.

Kwa kifupi, Uislamu wadai ya kuwa dini zote zilizotangulia zimefutiliwa mbali kwa sababu mbili. Kwanza, baadhi ya maagizo ya dini hizo yaliuhusu wakati ule ule tu, nayo yalikuwa sawa na hali za taifa au nchi au zama maalumu tu. Na hekima kamili ya Mungu ilitaka hayo yafutiliwe mbali na yapelekwe maagizo yaliyo sawa

na mahitaji ya mataifa yote na nchi zote na zama zote. Pili, maagizo hasa ya vitabu vya zamani yalikuwa yameharibiwa pia. Na vitabu hivyo havikubaki katika sura viliyokuwa nayo wakati viliposhuka. Na sasa ilikuwa vigumu kwa afuataye ukweli kuvitekeleza, kwani hivyo havikubaki katika sura viliyokuwa nayo wakati viliposhuka. Na sasa ilikuwa vigumu kwa afuataye ukweli kuvitekeleza, kwani hivyo havikuwa vyenye kumtuliza kwa sababu ya kutiwa shaka. Na juu ya vitabu hivi kuwa na mambo mengi ya ukweli humo ndani, mtu alikuwa hawezi kusema kwa yakini na utulivu kuwa amri anayotekeleza ndiyo iliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu ama sivyo. Basi, ili kuondoa wasiwasi na shaka iliyo kama sumu iangamizayo maendeleo ya kiroho, Mwenyezi Mungu akataka kushusha Neno Jipya na Sheria Mpya ambayo binadamu aweze kuifuata bila wasiwasi, ambayo kuhusu kila neno lake awe na hakika ya kwamba ni Neno la Mungu. Na hii pia ni tofauti kubwa kabisa baina ya Uislamu na dini zingine. Hakuna hata dini moja katika dini zingine ambayo vitabu vyake vya kidini vimehifadhika kama vilivyoteremka, au vina dalili wazi ya kuonyesha kuwa vimehifadhiwa. Lakini kuhusu kitabu cha dini ya Kiislamu, Kurani Tukufu, yawezekana kusemwa kwa yakini sawa na ushahidi wa historia, ya kuwa kipo katika sura yake ya asili kama kilivyomshukia Mtume[saw]. Hivyo, ule utulivu anaoupata Mwislamu aitekelezapo Kurani Tukufu, hawezi mfuasi wa dini

nyingine iwayo yote ile kuupata katika vitabu vyake vya kidini. Kwani, hali ya vitabu vingine vyote ndiyo hii ya kuwa ama imekwisha thibitika kwa ushahidi madhubuti wa historia kwamba haviko katika sura yake ya asili, ama vimepita katika zama za giza hata haiwezekani kusemwa ya kuwa vipo katika hali yake ya asili.

## Jibu la Upinzani: Kwa Nini Mwenyezi Mungu Hakulinda Vitabu vya Zamani?

Upinzani huu hauna maana ya kwamba kwa nini Mwenyezi Mungu hakuvilinda vitabu vya zamani? Kwani, katika siku zile za awali mataifa mbalimbali yalikuwa yametengana kwa umbali na utamaduni, hata ilikuwa haiwezekani kuyapelekea kitabu kimoja tu. Tena katika nyakati hizo hali yao ya kiroho pia ilikuwa ikipita katika daraja za kwanza. Kwa hiyo, ilibidi kupeleka manabii na vitabu mbalimbali kwa sehemu mbalimbali sawa na haja za nyakati hizo. Na kwa kuwa vitabu hivi vya zamani vilitakiwa kufutwa baada ya maendeleo ya binadamu, hivyo haja ya kuvilinda ilikuwa hakuna; ndiyo sababu katika Kurani Tukufn tu pekee mna madai haya ya kwamba:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحٰفِظُونَ

> "Hakika Sisi Tumeteremsha mauidha na hakika Sisi ndio Tuyalindao", (15:10).

Yaani, Mwenyezi Mungu mwenyewe atailinda Kurani Tukufu, wala hataiacha iharibiwe. Na hayo ndiyo madai

ambayo kitabu kingine hakikutangaza. Na kama kimedai, basi mtu yeyote atuonyeshe hayo madai katika kitabu cho chote. Sisi tutamtolea shukurani kwa hisani yake hii. Hakuna kitabu chochote kilichofunuliwa chenye madai kama hayo, wala hakiwezi kudai hivyo, isipokuwa Kurani Tukufu. Kwani, hakuna kitabu chochote, ghairi ya Kurani Tukufu, kilichodai kuwa ni kwa ajili ya dunia nzima na kimekamilika kwa kila jiha. Na kama kitabu bila ya kuwa na madai hayo mawili kingedai ya kwamba kitalindwa hadi siku ya kiyama, hapo muradi wake ungekuwa ya kwamba: Ama juu ya maendeleo ya utamaduni, na wanadamu kuchangamana kwa kimwili na kiroho, Mwenyezi Mungu alipenda (Mungu apishe mbali) kuwatenganisha wanadamu wote kwa kuwapa dini mbalimbali, na akataka kuwanyima ule umoja ulio msingi wa kupata maendeleo yote. Au ingebidi kukubali kuwa juu ya mwanadamu kuendelea mbele kwa kila jiha Mwenyezi Mungu hakumpa sheria iliyokamilika na akaziendeleza tu, bila haja na kinyume cha hekima, zile sheria zilizohusu nyakati mahususi na zama maalumu tu. Na mambo yote hayo mawili mtu mwenye akili hawezi kuyakubali. Basi, kwa kuwa vitabu vingine havikuwa kwa dunia nzima wala maagizo yake hayakuhusu namna zote za matendo ya binadamu, hivyo haikuwa lazima kuvilinda. Hali ya vitabu hivyo ilikuwa kama makambi yapigwayo mahali kwa muda tu wakati wa haja fulani. Haya makambi huwa hayalindwi jinsi yalindwavyo majengo yajengwayo kwa kuendelea

daima. Maana, makambi faida yake huwa kwa siku chache tu na baada ya kunufaika nayo haibaki haja yake. Lakini Majengo yanakusudiwa kukaa siku zote, hivyo kuyalinda huwa lazima.

## Madai ya Kurani

Kwa kifupi, ni dini ya Kiislamu tu miongoni mwa dini zote, ambayo kitabu chake kimedai kwamba ki kwa ajili ya wanadamu wote na zama zote zijazo, kama kisemavyo:

وَأُوحِيَ إِلَيَّ هَٰذَا الْقُرْآنُ لِأُنذِرَكُم بِهِ وَمَن بَلَغَ ۚ

'Na Kurani hii imefunuliwa kwangu ili kwayo niwaonyeni ninyi na yule imfikiayo', (6:20).[6]

Yaani, haikuwekwa sharti kwa kitabu hiki kwamba ni kwa zama fulani au nchi fulani tu. Kila atakayepata habari yake itamlazimu kukiamini na kukitekeleza. Kadhalika, Islam tu ndiyo dini ya pekee ambayo kitabu chake kilichofunuliwa kimedai:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا ۚ

'Leo Nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema yangu' (5:4).

Na matokeo ya lazima ya mambo haya mawili yalikuwa

[6] Kadhalika kinasema:

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿٢﴾

Mwenye baraka ni Yule Aliyeteremsha Furkani kwa Mtumishi wake ili awe Mwonyaji kwa walimwengu, (25:2)

ya kwamba ingesemwa kukihusu kitabu hiki ya kuwa Mwenyezi Mungu atakilinda. Kwa maana, hakuna haja kutangua kitabu kilichokwisha kamilika, wala hapana budi kukihifadhi kile kinachohusu zama zote.

## Tofauti Kati ya Uislamu na Dini Zingine

Katika maelezo yangu yaliyokwisha tangulia hapo mbele imedhihirika kuwa Uislamu wakubali kwamba dini zote zimetoka kwa Mungu. Lakini pia wadai ya kuwa ulipofika Uislamu, dini zote zilikuwa zimekwisha haribika. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu akateremsha Kurani Tukufu kwa kuongoza watu. Na kwa kuwa nguvu za kiroho za binadamu zilikuwa zimekwisha kamilika, na dunia vile vile ilikwisha endelea mbele mpaka kuweza kuungana pamoja, kama yalivyosadikisha matokeo ya baadaye, hivyo Mwenyezi Mungu akaipelekea dunia dini kamili ili kuipa maendeleo ya juu kabisa. Basi, sawa na kanuni hii, sisi tulinganishapo Uislamu na dini nyinginezo, twafanya hivyo ama kwa sababu dini hizo zilikuwa na mambo kadha mazuri lakini yalifutika baadaye kwa sababu ya zama nyingi kupita, au baadhi ya watu waliongeza ndani yake mafundisho kadha kwa kujitimizia baadhi ya makusudio yao. Au mafundisho ya dini hizo yalikuwa mazuri, lakini hayakuwa yenye kufaa kwa kila zama na kila wakati. Bali ndani yake, kwa kuangalia hali mahususi, mlitiliwa mkazo juu ya sehemu fulani tu ya tabia ya bindadamu

au faradhi fulani miongoni mwa faradhi za binadamu, na zikaachwa sehemu zingine au zikatajwa bila ya kutiliwa mkazo hata zisiweze kuathiri sawa sawa na kusawazisha matendo ya bidnadamu. Tofauti hii baina ya Uislamu na dini zingine, Kurani inaeleza kwa maneno haya:

وَ كَذٰلِكَ جَعَلْنٰكُمْ اُمَّةً وَّسَطًا لِّتَكُوْنُوْا شُهَدَآءَ عَلَى النَّاسِ وَ يَكُوْنَ الرَّسُوْلُ عَلَيْكُمْ شَهِيْدًا ؕ

'Yaani, na vivyo Tumewafanyeni umati bora ushikiliao njia ya katikati katika vitendo vyake; haupiti kiasi wala haupunguzi, bali vitendo vyake hukaa katikati kama kipimo cha mizani hata upande wowote hauachiliwi mbali. Tumewafanyeni hivyo ili muwe kama mashahidi kwa dini zingine na mataifa mengine. Yaani, kama vile ushahidi unaotolewa kuhakikisha ukweli uko wapi na u upande wa mtu gani, hivyo ndivyo wale miongoni mwenu watakaoonyesha ndani yao athari njema za maagizo ya Kurani Tukufu kwa kuyafuata, watakuwa kama mashahidi wa ukweli wake na athari zake nyingi ziletazo mabadiliko makubwa katika maisha ya kiroho, kwa mataifa mengine ambayo bado hayajasikia utamu wa ukweli wa Kurani Tukufu. Yaani wakiri kwa midomo na kwa vitendo ya kuwa wameyakuta madai yake kuwa sawa. Na watu, kwa kuona maisha yao matakatifu na msaada unaowateremkia kutoka mbinguni, wajue kwamba njia ya kweli ndiyo ile wanayoifuata hao. Na mwishowe,

amesema ya kuwa kama tulivyowafanya hao Waislamu wafuatao maagizoya Kurani Tukufu kuwa mashahidi juu ya mataifa mengine, ndivyo hivyo tulivyomfanya Mtume[saw] kuwa Shahidi juu ya kundi hilo. Yaani, kwa kuangalia maisha yake (Mtume[saw]) ukweli wa Uislamu waingia moyoni mwao.

Ilmuradi, Kurani Tukufu binafsi imedai ya kwamba Dini ya Kiislamu inao ubora huu juu ya dini nyigine ya kuwa ndani yake hakuna kupita kiasi wala kupunguza kuhusu jambo lolote lile. Bali maagizo yake ni ya katikati, na kwa hiyo yanafaa kwa kila zama na kila nchi na kila taifa katika kila hali. Na ingawaje katika Kurani Tukufu mmetajwa mamia bali maelfu ya mambo mazuri kama hayo, na katika Hadtihi za Mtume[saw] pia mazuri mengi yanapatikana, lakini kwa wakati huu nitaeleza kwa kifupi uzuri mmoja tu ambao kwao itajulikana ya kuwa sasa ni dini ya Kiislamu tu pekee iyatimizayo mahitaji yote ya binadamu. Hakuna amri iliyoletwa kwa haja na zama maalumu tu ambayo haifai baadaye. Hakika, hii pekee ndiyo dini ambayo watafutao ukweli wanatakiwa kuikimbilia na kuinunua hata kwa kuuza uhai wao. Kwani, kwa mtu mwema hakuna kitu kipendwacho zaidi kuliko ukweli.

Katika malinganisho haya mafupi nitatia mkazo zaidi juu ya mambo mazuri ya Uislamu, na nitatosheka kuashiria tu kwenye amri za dini nyingine zilizokwisha

haribika au ambazo kuzitekeleza katika kila zama na kila hali hakuwezekani. Maana, kwanza, hakuna nafasi; pili, pengine watu wengine watafadhaika kwa maelezo yake.

## Kusudio la Dini

Kabla ya kulinganisha Uislamu na dini zingine kwa njia hii maalumu niliyokwisha eleza hapo juu, yapasa kujua ya kuwa kusudi la dini huwa nini, ili iweze kufikiriwa ya kwamba kwa kutimiza makusudio hayo dini ipi imefuata njia ya katikati? Kurani Tukufu yaeleza makusudio mawili tu ya dini: Kwanza kutimiza haki za Mwenyezi Mungu, na pili, kuangalia haki za watu. Dini zingine vile vile hazipingani na Kurani Tukufu katika jambo hili. Basi katika malinganisho haya twaangalia makusudio hayo mawili.

# KUUNGANA NA MWENYEZI MUNGU

## Uhusiano wa Kimoyo Hupatikana kwa Sababu Gani?

Katika malinganisho haya, kwanza kabisa twachukua kuungana na Mwenyezi Mungu na kufikiria kwamba Uislamu umeweka taratibu gani ili kusimamisha mwungano kati ya Mwenyezi Mungu na binadamu. Lakini kabla ya kueleza taratibu hizo zilizoshikwa na Uislamu kwa kuunganisha binadamu na Mwenyezi Mungu, yatupasa kuangalia, ili kurahisisha zaidi madhumuni haya, ya kuwa katika bindadamu mna nguvu gani zilizofichika ambazo ndizo sababu za uhusiano wa kimoyo kupatikana baina ya mtu na kitu kingine, na ya kuwa chini ya amri za nguvu gani yeye humtii aliye mkuu mno kuliko yeye.

Ikumbukwe, basi ya kuwa binadamu huhusiana na kitu kingine kwa moyo kwa sababu ya jazba mbili tu: kwa sababu ya kukipenda ama kukiogopa. Tazameni namna zote za urafiki na uhusiano. Sababu yake ni ama upendo au hofu. Binadamu, pengine, anakuwa na mapenzi ya kitu fulani, basi, kwa sababu ya haya mapenzi yeye anahusiana nacho. Anafurahi kukiona wala hapendi kutengana nacho. Anajitahidi kukikaribia mpaka anaanza kulichukia jambo limdhurulo mpendwa wake au asilolipenda huyo mpendwa; na hupenda kitu au kazi anayoipenda mpendwa wake au inayomnufaisha yeye.

Ilmuradi, kwa sababu ya upendo, yeye anaanza kukipenda kila anachopenda mpendwa wae, na kukichukia kila anachokichukia yeye. Na upendo huu ukiendelea sana, basi hufikia hali ya kuwa kumridhisha mpendwa wake inakuwa ni tabia yake ya pili. Anafikiria ya kwamba ni tabia yake hasa kuzipenda baadhi ya kazi fulani na kutokuzipenda baadhi nyingine. Lakini, kuzichukia hizo au kupenda nyingine, kwa hakika, huwa kivuli tu cha fikira za mpendwa wake.

Kadhalika, twaona baadhi ya uhusiano unakuwa kwa sababu ya hofu tu. Hofu ikiondoka, basi mara moja uhusiano huu wakatika. Kwa mfano, baadhi ya watu wanafuga wanyama wakali na kuwazoesha nao. Lakini, mara nyingi imeonekana ya kuwa uhusiano wao na wanyama hao wakali unakuwa wa hofu tu; ndiyo maana wanashika mjeledi au upanga wakiwaendea. Na imetukia mara nyingi ya kwamba ikiwa wakati fulani walisahau kuchukua mjeledi au upanga na wakamwendea huyo mnyama mbuai, basi akawashambulia na kuwaua au kuwajeruhi. Hiyo ndiyo hali ya baadhi ya wanadamu wenye tabia ya kinyama ya kwamba hawatii kwa mapenzi na huruma. Wapo wengi wanaowapiga wazazi wao na kuwadharau ambapo hisani zao juu ya mtu huwa nyingi mno kuliko wanadamu wote. Baadhi wengine wanapobalehe, wanawapa sumu wazazi wao ili kurithi mali yao. Lakini hao hao hawatamki neno mbele

ya watawala na wanawatii kwa nje, na wanakuwa mbele yao kama mtoto aonaye haya. Huu uhusiano na utii wao unakuwa kwa sababu ya kufikiria ya kuwa ikiwa tutavunja kanuni kwa dhahiri tutaadhibiwa. Waila kama watawala na serikali ingetaka kuwatiisha kwa huruma na mapenzi tu, wangejitenga nayo siku hiyo hiyo na kuanza kupambana nayo. Hivyo kwa kuangalia tabia ya binadamu inajulikana kuwa uhusiano hupatikana kwa sababu mbili tu: ama kwa upendo au kwa hofu.

## Sababu za Upendo

Tukiangalia sababu za upendo kupatikana, inaonekana ni kwa sababu mbili: Ama uzuri au hisani. Yaani, mwanadamu anakipenda kitu fulani, pengine kwa sababu chaonekana ni kizuri kwa sura, huluka, elimu au fahamu. Ilmuradi, uzuri uwe wa namna yoyote, baadhi ya wanadamu wanajitolea kwake. Majumba yaliyopambwa, picha, mahali penye majani na baadhi ya maua yenye rangi nzuri yasiyo na harufu ni miongoni mwa vitu vya kuonekana, waila havifaidi, bali vyataka gharama. Kadhalika, wanadamu wanawapenda watu wazuri. Na uzuri huwa wa namna mbalimbali kama ilivyokwisha elezwa hapo juu. Pengine sura zao zinakuwa nzuri na pengine huluka na elimu na akili au sifa zao zinakuwa nzuri; hivyo watu wanawapenda. Sababu ya pili ya mapenzi ni kupatikana kwa ‘hisani’. Uhusiano mwingi wa mapenzi hupatikana kwa sababu

ya hisani. Basi sababu moja kubwa ya mapenzi kwa wazazi ni hisani pia wanazomfanyia mtoto tangu kuzaliwa kwake mpaka aanzapo kufanya kazi. Kadhalika mtumishi anampenda bwana wake mhisani, na bwana anampenda mtumishi wake mwaminifu. Uaminifu vile vile ni namna mojawapo ya hisani. Kwani uaminifu ndio malipo ya hisani, na malipo ya hisani yaweza kuwa nini isipokuwa hisani tu? Ndivyo hivyo yalivyo mapenzi baina ya mume na mke. Kwao mapenzi hupatikana kwa sababu zote mbili, za uzuri na hisani. Ilmuradi, uhusiano wote wa upendo huwa matawi ya uzuri na hisani. Na mapenzi baina ya ndugu pia huwapo kwa njia hizo mbili; kwani, hayo mapenzi huwa kwa sababu ya upendo mwingine. Na kwa hakika sababu yake ni ule uhusiano wa watoto ulio kwa wazazi. Na kwa kuwa ndugu na dada wanakuwa wapendwa wa mpendwa mmoja, bali sehemu ya mwili wake, hivyo, kwa tabia, ndugu mmoja humpenda nduguye mwingine au dada yake; wala hajui mara nyingi ya kwamba sababu ya hayo mapenzi i nini?

Ilmuradi, sababu ya upendo ndio uzuri au hisani. Na uhusiano wa hisani unagawanyika tena katika sehemu mbili. Ama mtu anapendwa kwa sababu ya hisani yake au anawapenda wengine kwa sababu anayo tabia ya kuwafanyia wengine hisani. Huu upendo unakuwa ni huruma na ukarimu ambao ni matokeo ya tabia ya hisani.

Tuangaliapo zaidi tabia ya binadamu, twajua ya kuwa baadhi ya watu wanazo sifa hizo zote tatu. Yaani, uhusiano wao unakuwa wa namna zote tatu. Uhusiano mwingine kwa sababu ya hofu, na mwingine kwa sababu ya kupenda uzuri, na mwingine kwa sababu ya kupenda hisani. Lakini, katika baadhi yao sifa moja au mbili zafutika kwa sababu fulani. Yaani, hao wanakuwa na uhusiano kwa sababu ya uzuri tu au hisani tu au hofu pekee; jazba nyingine haitaharaki ndani yao. Wapo watu ambao maadamu mtawatumikisha kwa mapenzi watafanya kazi kwa furaha, lakini watasimama kupambana watakapokaripiwa au kutishwa. Baadhi ya watu hawatajali sababu zote mbili za upendo, yaani ya uzuri na hisani, lakini watakuwa watii mara moja kwa kutishwa.

Baada ya kuchungulia huku kwa tabia ya binadamu, twalazimika kukubali ya kuwa mafundisho yale tu yaweza kufaa kwa kila zama na kila nchi na kila binadamu ambayo ndani yake njia ya kuleta mwungano ipatikane kwa kutaharakisha jazba hizo zote tatu. Kama ipo dini itiliayo mkazo uzuri tu wa Mwenyezi Mungu na kumwita binadamu kwenye upendo ambao sababu yake siyo matamanio au kutaka neema fulani, wala hakuna matamanio ya kupata malipo, basi, dini hii yaangalia kundi moja tu la watu. Lakini, makundi mengine mawili ambayo hayawi na uhusiano bila ya hisani au hofu, ambayo ndani yao jazba hii imekufa kwa sababu fulani,

njema au mbaya, inayohimiza upendo kwa sababu ya uzuri tu pekee na kuleta mwungano kwa njia hiyo, basi, hayo makundi hayawezi kumfikia Mwenyezi Mungu kwa njia ya dini hii. Na lazima wao kwa kukosa dawa yao wajitenge na dini na kuangukia maangamio ya daima.

Kadhalika, ikiwa dini fulani inatia mkazo juu ya hisani pekee na yataka kumwunganisha binadamu na Mwenyezi Mungu kwa kumwelekeza kwenye neema zake anazowapa watu wanaoungana naye, basi hii dini pia yaelekea upande na kuacha njia ya katikati. Na zile tabia ambazo huungana na Mwenyezi Mungu kwa njia ya uzuri na hofu, dawa yake haiko ndani ya dini hiyo: na tabia zote za namna hii haziwezi kuletwa kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya dini hii. Kadhalika, kama dini fulani inatilia mkazo hofu tu ya Mwenyezi Mungu, na inamweka mbele ya dunia kwa sura ya kutisha wala haitumainiwi kupata kwake msamaha au huruma, basi watu wanaoathirika mioyoni mwao kwa hofu wataweza kunufaika kidogo kwa dini hii. Lakini haziwezi kufaidika na dini hii zile tabia zilizozoea kuungana kwa upendo. Na watu waunganao kwa sababu ya kuogopa, mwungano wao huwa kwa muda mdogo tu, wala hastahili mtu kupewa neema ambazo mwungano wa upendo wamstahilisha kupewa hizo.

Basi, ile dini inayotaka kusuluhisha dunia kwa kusema "Mungu ni Upendo", na yategemeza ukombozi juu ya

kuamini tu itikadi fulani na inasahau kabisa upande wa matendo, haiwezi kamwe kumtosheleza binadamu. Kwani, wapo wengi watakaoshindwa kwa tabia yao ya kikatili ikiwa watategemea imani tu. Na upendo wa Mwenyezi Mungu ukiwekwa mbele yao kwa njia hata nzuri namna gani hawataathirika kwao na watajitenga mbali na Mwenyezi Mungu kama wenye bahati mbaya wanaoona hisani za wazazi wao lakini tena wanawaasi.

Kadhalika, ile dini isemayo kuwa Mwenyezi Mungu anapendelea upande mmoja tu, yaani anahusiana na taifa moja tu, na neema zake maalumu zote hupatikana kwa kuhusika na kizazi mahususi tu, haiwezi kamwe kuwa yenye kusuluhisha dunia nzima. Kwani, dini kama hiyo inawatilia wanadamu mioyoni mwao chuki juu ya Mwenyezi Mungu, sio upendo.

Tena, ile dini yenye itikadi ya kuwa Mwenyezi Mungu hasamehi kabisa dhambi yoyote wala hana uwezo huo, ingawaje ikiri kwa midomo kuwa Mungu ni Mwenye huruma kama wazazi au hata zaidi kuliko hao, lakini, dini kama hiyo haiwezi kuwa kutoka kwa yule Mwumba wa tabia ya asili ya binadamu ambaye ametia huruma katika nyoyo za wanadamu kwamba wao wawasamehe wanaowakosea hata kama wamekwisha kuwatia hasara. Lakini, Mwenyezi Mungu hapati dhara kwa sababu ya kitendo chochote cha binadamu.

Kadhalika, ile dini inayosema ya kuwa Mwenyezi Mungu anapomwokoa mtu, humbakizia baadhi ya

madhambi yake na kumrudisha tena duniani kwa kumwadhibu juu ya dhambi hizo haiwezi kuwa njia ya kumwunganisha yeye na Mwenyezi Mungu. Kwani, kwa sababu ya itikadi hii hupatikana chuki juu ya Mwenyezi Mungu, na papo hapo mwanadamu kwa kukata tamaa anajasiri zaidi kufanya madhambi.

Basi, kwa hakika, dini ile tu yaweza kuwa kwa ajili ya dunia nzima ishikayo njia ya katikati katika mambo hayo yote. Upande mmoja, inapendwa na dunia kwa kuieleza uzuri wa Mwenyezi Mungu, na inachochea jazba ya upendo wake kwa kumkumbusha binadamu hisani zake za zamani na mpya. Na upande mwingine, inamlazimisha kuungana na Mwenyezi Mungu kwa kueleza vizuri sana enzi yake na nguvu yake na kuchukia kwake maovu. Na dini hiyo ndiyo Islam tu pekee.

## Katika Uislamu Mna Dawa ya Mtu wa Kila Tabia

Ndani ya Sura ya kwanza kabisa ya Kurani Tukufu, anayoisoma Mwislamu katika kila sala, imo tiba kwa mtu wa kila hali. Humo yameelezwa madhumuni hayo hayo. Mwenyezi Mungu anamfundisha mja wake kutamka:

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ اِيَّاكَ
نَعْبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُ

Yaani, naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. Sifa zote njema na uzuri wote na urembo wote unaostahili kusifiwa unapatikana katika Mwenyezi Mungu. Tena, yeye si Mzuri tu, bali ni

Mfanya hisani vile vile. Yu Mola wa walimwengu wote, kwani ameumba vitu vyote na roho zote kisha anavilinda kimoja kimoja au vyote kwa jumla. Na kwa njia ya kila namna anavifikishia ukamilifu wake kwa kukuza nguvu zake taratibu. Yu Mwenye hisani mno; si kwamba anatoa tu malipo ya mtumishi, bali humnyeshea mvua ya fadhili zake bila yeye kufanya kazi au utumishi wowote. Na hakomi hapo. Bali, wale watu wamtoleao shukurani juu ya fadhili zake wazipatazo kutoka kwake na wakazitumia ipasavyo kuzitumia, basi kwa sababu ya kufanya hivyo pia anawanyeshea mvua ya fadhili zake. Na baada ya kumlipa mwanadamu sawa na kazi yake anampa bakhshishi vile vile. Mungu ni Mmiliki wa siku ya malipo. Yaani, siyo tu ya kwamba yu Mzuri sana na Mwenye hisani, bali hupima vitendo vyote vya mwanadamu katika wakati maalumu, kisha kwa uwezo wake mwenywe anamneemesha na kumwadhibu mwenye shari hapa duniani na huko Akhera vile vile. Katika neno 'Mmiliki' ameashiria ya kuwa neema yake huwa kubwa na adhabu yake huwa kali, kwani, asiyekuwa Mmiliki, mtu anaweza kuepuka adhabu yake. Kwa mfano, kama mfalme akitaka kumwadhibu mtu fulani naye anakufa au anajiua kwa kufikiria adhabu ya taabu sana, basi ataepuka adhabu ya mfalme huyo. Lakini, Mungu amesema: Sisi Tuna mamlaka kamili wala hakuna awezaye kuponyoka katika mamlaka yetu. Basi, hata kama hakuna jambo lolote

liwezalo kuwa sababu ya kuunganisha nyinyi nasi, jueni, basi, ya kuwa sisi tunatoa adhabu kali juu ya kuhalifu amri yetu.

Anaendelea kusema:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَ إِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

> Wewe tu twakuabudu, na Wewe tu twakuomba msaada.

Yaani, binadamu hata kama awe wa tabia gani — akiwa mwenye kupenda uzuri ama mwenye kuamini kwa kuangalia hisani au kwa hofu — afikiriapo sifa hizi zote, hupata katika sura Fatiha dawa sawa na tabia yake, na bila kuweza kujizuia husema: Ee Mungu, mimi ninakutii wewe tu. Yaani, ambapo mambo yote yale yaliyo sababu ya dhati fulani kupendwa yanapatikana kwako, basi, tena, naweza huungana na nani kama si wewe?

Katika maneno haya imeelezwa ya kuwa mumini aunganapo na Mwenyezi Mungu kwa utimilifu, basi, upendo wake na hofu yake hufungamana na yeye tu; tena hamshirikishi yeyote na Mwenyezi Mungu katika mapenzi wala hofu. Kama yeye anapenda kitu, ni kwa ajili ya Mungu na akiwa ndani mwake; na akiogopa basi ni kwa sababu ya amri ya Mungu. Na anaviogopa vile tu ambavyo yeye amemwamrisha kujilinda na kuviharibu. Na kwa kuwa mtu azifikiriapo sifa hizi zilizokamilika anabaki hajitambui kwa sababu ya mapenzi na hofu,

nayo yanamghilibu kiasi hiki ya kwamba sasa anajifikiria dhati yake kuwa duni na kama maiti mbele ya Mwenyezi Mungu. Na ili kueleza fikira hii Mwenyezi Mungu ameongeza kusema:

وَ اِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُ

Na Wewe tu twakuomba msaada. Yaani, baada ya kujua uzuri na hisani na utukufu wako hatuwezi kujitegemea nafsi zetu ya kuwa zitaweza kutimiza mapasiko ya mapenzi na uhusiano wa hofu yanayotulazimu kwa kuungana nawe. Kwa hiyo, twakuomba msaada wewe tu ya kuwa utujaalie uwezo wa kutimiza wajibu wa mwungano huu.

Katika maneno haya machache uzuri wa Mwenyezi Mungu na hisani yake na utukufu wake vimeelezwa bayana mno hata watu wa nchi yoyote, taifa lolote, utamaduni wowote na zama yoyote hawana budi kuathirika navyo. Na kila mtu moyo wake unalazimika kuungana na Mwenyezi Mungu afikiriapo sifa za Mungu kwa kuangalia aya hizo zilizoelezwa sasa hivi.

## Njia ya kukamilisha Uhusiano wa hofu

Pamoja na hayo yafaa kukumbuka hapa ya kwamba ijapokuwa hofu vilevile ni njia mojawapo ya kuleta mwungano, lakini njia hii ni duni sana kwa kuleta mwungano; kwa maana uhusiano wa hofu hauwi uhusiano wa kikweli. Lakini pia hakuna shaka katika

neno hili ya kuwa baadhi za tabia haziungani ila kwa sababu ya hofu tu kama ilivyoelezwa hapo juu. Na Kurani Tukufu imeeleza njia moja ya kukamilisha huu uhusiano pia, na imeiweka hofu kuwa hatua ya kwanza tu ya kuleta mwungano.

Twaona kuwa baadhi ya watoto wasipokwenda shuleni au hawatekelezi baadhi ya mambo ya lazima, basi, wazazi wao waelewapo ya kuwa mapenzi yao na hisani zao haziwezi kusuluhisha tabia za wana hao, basi wanawapeleka shuleni kwa kutumia ukali. Na kwa muda kadha watoto wanaendelea kwenda shuleni kwa sababu ya hofu waitiayo wazazi wao mioyoni mwao. Lakini, kama yupo mwalimu mpole, katika siku chache tu anatia mapenzi yake mioyoni mwao, kisha hofu ile inageuka kuwa mapenzi. Na ingawaje, walianza kwenda shuleni kwa sababu ya hofu, lakini, baadaye mapenzi yanachukua mahali pa hofu. Hivyo hatari ya matokeo mapungufu ambyo yangepatikana kwa sababu ya mafunzo kwa hofu inatoweka. Ndivyo hivyo Mwenyezi Mungu amtendeavyo mtumishi wake. Na ijapokuwa mwanadamu amekumbushwa utukufu wa Mfalme wa ardhi na mbingu na ukali wa kamato lake vile vile ili kuwaongoza wanadamu wote pamoja na kuwaokoa wale ambao kwa sababu ya upungufu fulani hubadilika hivi kwamba hawasogei karibu ila wanapotishwa, lakini anasema Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu:

وَرَحۡمَتِي وَسِعَتۡ كُلَّ شَيۡءٖۚ

"Na rehema yangu hukienea kila kitu." (7:157)

Sasa, mkisoma yaliyoelezwa hapo juu kwa kuyalinganisha na muradi wa aya hii, mtaona ya kwamba hofu imefanywa kuwa hatua ya kwanza peke yake.

Lakini mtu amjiapo Mwenyezi Mungu kwa hofu, yeye humnyeshea mvua nyingi ya rehema yake na kumnyunyizia fadhili zake. Ijapokuwa mtumishi wake huyo anaendelea kuweka msingi wa uhusiano wake juu ya hofu, lakini, mwishowe ugumu wa moyo wake unatoweka; na pole pole anahisi moyoni mwake kwanza hisani ya Mwenyezi Mungu, kisha uzuri wake. Na uhusiano wa hofu unageuka kuwa uhusiano wa upendo; na moyo wa mtu unajaa ukumbusho wa rehema ya Mwenyezi Mungu badala ya kujaa hofu. Na mwishowe rehema halisi inabaki na mapenzi matupu yanaonekana. Naam, hofu inayobaki juu ya mtu huyu ni kwamba asitengane na Mpendwa wake wa pekee kwa sababu ya kitendo chake fulani.

## Njia Uliyotumia Uislamu kwa Kuleta Mwungano na Mwenyezi Mungu, Dini Zingine Haziwezi Kuleta Mfano wake

Hayo yaliyoelezwa hapo juu yanadhihirisha taratibu zilizoshikwa na Uislamu kwa kumwunganisha binadamu na Mwenyezi Mungu na kuuimarisha mwungano huu. Kila mtu anaweza kuelewa kwa kuchungulia kidogo tu ya kuwa namna gani njia ya

katikati imeshikwa katika taratibu hizo. Zimeangaliwa humo pande zote zile ambazo zinaweza kuwa njia ya kumwunganisha mtu na Mwenyezi Mungu. Lakini, maagizo yaliyotolewa na dini zingine kuhusu jambo hilo, si mapana namna hii wala hayaafikiani na kila tabia. Kwa mfano, dini ya Kiyahudi imemdhihirisha Mungu katika sura ya kutisha mno, na imetia mkazo sana juu ya hasira yake na tamaa yake ya kujilipiza kisasi. Sababu yake ilikuwa hii ya kwamba wana wa Israeli, kwa kutawaliwa na Firauni aliyekuwa mfalme mdhalimu, walikuwa wamezoea kutii kwa kutishwa na kudhulumiwa. Basi, Mwenyezi Mungu akadhihirika kwao kwa ngurumo na matetemeko. Lakini, pole pole tabia za Wayahudi zikawa sawasawa. Na baada ya muda kadha walipita kiasi katika kutawaliwa na fikira hizo. Ndipo ikabidi kuwa sawa na hali iliyopo Yesu alete Ujumbe wa Upendo, na Roho Mtakatifu adhihirike kwa sura ya njiwa ambaye ni ndege mpole na mlainifu wa moyo, na utiliwe mkazo upendo wa Mwenyezi Mungu ili kusahihisha mawazo yasiyokuwa sawa ambayo yalienea kati ya Wayahudi kuhusu ukali wa Mwenyezi Mungu na tabia yake ya kujilipiza kisasi. Basi, udhaifu wa wakati ule ulitibiwa kwa njia hii. Lakini, baada ya muda kadha maelekeo ya Wakristo yalikwenda upande kabisa na wakaanza kughafilika na matendo. Hivyo, sheria nyingine ikahitajika.

Hivyo ndivyo ilivyo hali ya dini zingine. Katika dini moja ilionekana haja ya kutia mkazo juu ya sifa za Mwenyezi Mungu za kughadhibika na kuadhibu; na dini nyingine imetia mkazo juu ya mapenzi na upendo wake. Na kwa kuwa mafundisho yote hayo yalikuja kwa muda tu, basi, hali ilipogeuka yakawa yenye kudhuru badala ya kufaidisha. Na kwa kuwa sasa wakati uliopendw na hekima kamili ya Mwenyezi Mungu uwe wa kupeleka dini kamili na kwa dunia nzima ulikuwa umefika, basi Bwana wa manabii na kiongozi wa watawa — Muhammad[saw] — aliteremshiwa wahyi uliokusanya ndani yake mambo yote mema. Haukuwa na nafasi ya kuongezewa lolote lile. Mahitaji ya watu wa tabia, elimu na ustaarabu mbalimbali hayakupuuzwa. Jambo lisilohitajiwa au lililo la kitambo tu halikuingizwa ndani yake. Baadhi ya wajinga hudhihirisha uchafu wao kwa kutukana watakatifu wa Mwenyezi Mungu, lakini sisi hatuwafuati na hatusemi ya kuwa dini zote zilizoutangulia Uislamu zilikuwa za uwongo; bali twazisadikisha. Naam, matukio na kupenda kwetu ukweli kwatulazimisha tukubali ya kuwa ukamilifu ulioko katika Uislamu, hauko katika dini nyingine yoyote. Baada ya Uislamu kufika, sasa hakuna haja ya dini nyigine. Njia zilizotumiwa na dini hizo kwa kuleta mwungano na Mwenyezi Mungu zilikuwa sawa kwa wakati ule. Lakini, sasa, katika zama hizi ambapo maendeleo ya utamaduni yameifanya dunia kuwa kitu

kimoja, na elimu za binadamu zimeendelea mbele sana, njia hizo haziwezi kutosheleza kwa kumwongoza mwanadamu. Ni Uislamu tu, sasa, unaoweza kuongoza dunia nzima kwa maagizo yake yasiyo na ila. Maagizo yake hayatii mkazo juu ya jambo fulani tu mahususi, bali yaeleza miongozo yote iliyohitajiwa. Dini zingine zina mambo kadha ya kweli, lakini hakuna dini iliyokusanya ndani yake uzuri wote upatikanao katika Uislamu.

Leo hakuna dini yoyote juu ya ardhi, isipokuwa Islam, inayoweza kumwunganisha binadamu na Mwenyezi Mungu. Maadamu Mwenyezi Mungu amekwisha leta sheria iliyokamilika, basi sasa amefunga milango yote ya kudhihirisha radhi yake isipokuwa Uislamu. Na, sasa, mtu hawezi kumfikia Mwenyezi Mungu mpaka ajitwike nira ya Uislamu shingoni mwake.

Nasikitika kuwa haiwezekani kueleza kwa kirefu madhumuni hayo kwa sababu ya nafasi ndogo. Kama si hivyo, ningetoa mifano mingine kwa kueleza ya kwamba ili kusimamisha mwungano na Mwenyezi mungu, Uislamu umetumia taratibu ambazo dini nyingine hazikutoa mfano wake.

## SEHEMU YA PILI

## Kuwahurumia Viumbe vya Mwenyezi Mungu

Kama nilivyokwisha eleza hapo juu, dini ina kazi nyingine vile vile zaidi ya kumwunganisha binadamu na Mwenyezi Mungu. Nayo ni kuwafunza wafuasi wake kuvihurumia viumbe vya Mwenyezi Mungu. Baada ya kumaliza sehemu ya kwanza, naeleza mafundisho ya Uislamu yanayohusu jambo hili.

Maelezo kuhusu huruma kwa viumbe vya Mwenyezi Mungu yana sehemu tatu: Kwanza, mtu kujitendea nafsi yake; pili, mtu kuwatendea wanadamu wengine; tatu, binadnmu kuwatendea wanyama.

Katika sehemu hizi tatu, kwanza kabisa naeleza ya kuwa Uislamu umemwamrisha binadamu kujitendea nafsi yake namna gani.

### Mtu Kujitendea Nafsi yake

Dini mbalimbali zimesema sana juu ya wanadamu kutendeana wao kwa wao. Lakini maagizo kuhusu jambo hili ya kuwa mtu anatakiwa kujitendea nafsi yake namna gani yanapatikana katika dini chache sana. Uislamu umeeleza jambo hili pia kwa uwazi sana; na zaidi ya kumwonyesha binadamu njia za kiroho za kumfikia Mwenyezi Mungu, umemwongoza ajitendee vipi nafsi yake. Na masala haya ni ya muhimu sana na dini yoyote haiwezi kukamilika bila ya kueleza haya.

Mwanadamu hawezi kusuluhika barabra asipoambiwa namna anayotakiwa kujitendea nafsi yake. Maana, mwili hupata athari kwa roho, na roho haina budi kuathirika na hali mbalimbali za mwili. Tunaona mtu apigwapo mwilini, roho yake pia huudhika sana na moyo wake huhuzunika. Na inatukia mara nyingi ya kuwa kwa sababu ya pigo kali inatokea tofauti katika hisia za binadamu. Na pengine kwa matokeo ya huzuni nyingi mwili unaanza kukonda na katika nafasi ya saa chache tu mtu anakuwa mnyonge. Kwa mfano, mara nyingi imetukia ya kwamba mtu fulani alipopata msiba mkubwa mno, nywele zake zikawa mvi katika saa au siku chache tu.

Ilmuradi, kwa mazoea yetu tunajua kuwa Mwenyezi Mungu amefungamanisha mwili na roho hivi kwamba kila kimoja katika hivi viwili kinaathiri kingine mara moja. Basi, ikiwa hali ya kukaribiana kwa mwili na roho ni hivyo, ni lazima tena ya kuwa hali ya maendeleo ya kiroho itafuatana na hali ya kimwili. Na ile dini ambayo haimwelezi mwanadamu ajitndee nafsi yake namna gani, kwa haki,a inamwacha katika kizingia cha maji ili aangamie. Na ile dini inayotoa maagizo nusu-nusi kuhusu jambo hilo, maagizo hayo yaweza kuwa sawa katika hali fulani, lakini si kwa ajili ya kila mtu, bali aghlabu yatakuwa sababu ya kuwaangamiza wengi. Twaona baadhi ya dini zafundisha kuwa kiasi mwili

unachoadhibiwa, kiasi hicho hicho maendeleo ya roho yatapatikana. Matokeo ya mafundiho hayo yamekuwa kwamba wafuasi wa dini hizo wanajaribu sana kuvunja nguvu zao za kimwili na wanatumia njia ambazo kwazo waiangamize kabisa miili yao. Baadhi ya watu wanashinda katika kiangazi karibu na moto uwakao, nao wanaharibu wenyewe nguvu zao zote za kimwili. Kadhalika, katika kipupwe wao wanaendelea kukaa katika maji baridi. Wengine, mara jua litokapo, wanasimama wakilielekea na wanaendela kulitazama bila kupepesa macho mpaka lichwe. Kwa njia hii wanapoteza bure mchana kutwa wenye nuru ambao Mwenyezi Mungu aliumba kwa ajili ya kufanya kazi humo. Wengine tena, wanashinda wakati wote wakining'inia kichwa chini miguu juu na wanaliona hilo hilo kuwa ni wema mkubwa. Wengine wanajiondoa katika uanadamu kwa kujihasi. Wengine, kwa shabaha ya kuua tamaa za nafsi, wnajihadhari na vyakula vizuri, nao wanaacha kutumia vyakula vyote vizuri. Na hata kama wakila kitu chochote kizuri wanatia ndani yake kitu kama majivu na vinginevyo. Kwa njia hii wanataka kuua tamaa mbaya za nafsi zao. Wengine wanakaa kimya daima, na kwa njia hii wanataka kumkaribia Mwenyezi Mungu. Wengine hata wanakula uchafu, na wengine wanakula mzoga wa mtu. Wengine wanafunga saumu kila siku. Wengine wanafunga nia ya kwamba hawataoa maisha mazima, na wanaume wengi na

wanawake wanakaa hivi hivi maisha yao yote. Wengine wanaacha kuoga na kukata kucha na mambo mengineyo ya usafi. Ilmuradi, kuna mambo mamia na mamia ya namna hii yaliyoagizwa na dini mbalimbali nayo yanapendwa, na wayafanyao hayo wanafikiriwa kuwa wateule na wapendwa wa Mwenyezi Mungu. Lakini, kwa hakika, huu ni ukatili wanaofanya hao watu kwa nafsi zao. Wanakuwa watu wasiomshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake. Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu mikono ya kushikilia, mdomo kuzungumzia, macho ya kutazamia na miguu kutembelea; na hivyo vyote ni neema zake. Basi anastahili kulaumiwa namna gani yule mtu asiyetumia hizi neema za Mwenyezi Mungu, wala hazithamini kitu! Mtu wa namna hii anamwondolea Mwenyezi Mungu heshima; kwani anaitupilia mbali neema yake kwa kuipuuza kwamba siipokei. Hii ni dhuluma vile vile juu ya nafsi yake, kwani anajitesa bila sababu na pasina faida yoyote. Kadhalika, wale wanaoazimia kukaa maisha yote bila kuoa, au wapotezao wenyewe nguvu zile zenye kuendeleza kizazi cha binadamu, wanajidhulumu nafsi zao kwa kujizuia wasiwe na jazba hizo takatifu alizowajaalia Mwenyezi Mungu. Matendo kama hayo hayawezi kumpendeza Mwenyezi Mungu, kwa maana anayekatalia mbali neema yake hawi mpendwa wake abadani. Hivyo, wale ambao hawatumii vitu vizuri au wanaotumia uchafu, wao pia wanajifanyia nafsi zao

ukatili usio na mipaka. Hao wote, badala ya kumwepuka Shetani, mara nyingi wanajitia katika mtego wa Shetani. Kwani, matokeo ya kuudhi mwili yatakuwa kwamba roho yake pia itapata udhia. Basi akili yake itakuwa nzito hata hataweza kufahamu mambo magumu. Ama namna fulani ya kichaa itapatikana ndani yake. Hivyo, yeye atanyimwa kabisa zile neema zilizowekwa kwa wamwabuduo Mwenyezi Mungu. Historia sahihi kuhusu watawa wote waliopita duniani haithibitishi ya kuwa walipoteza nguvu zao namna hii. Naam, yawezekana kwamba kwa kuona nafsini mwa baadhi ya watu msukosuko wa tamaa mbaya, hao (watawa) waliwaamuru kufanya baadhi ya kazi ngumu za namna hii kwa kusikia haja kwa kitambo tu ya kupoza msukosuko huo. Lakini, agizo lolote la namna hii haliwezi kupenya katika dini iliyo kwa ajili ya ulimwengu mzima, kwani kuyaeneza hayo maagizo ndiyo kumnyima binadamu maendeleo yote anayopata kwa sababu ya elimu Aliyomjaalia Mwenyezi Mungu. Hebu, fikirini kidogo, kama wenyeji wote wa nchi fulani wakiachilia mbali kazi zote na wakaning'inia vichwa chini miguu juu kwa kufunga kamba mitini, au wakikatakata miti msituni na kukaa ndani kwa kuwasha moto pembezoni mwao, au wakifunga ahadi mabwana na mabibi wote kwamba kwa ajili ya Avtar au Nabii fulani tutakaa bila kuoa maisha mazima, wala hatutafunga ndoa, basi, hali ya taifa hilo au nchi hiyo

itakuwaje? Je, kuna shaka katika jambo hili ya kuwa katika miaka michache tu nchi hiyo itaangamia na wanyama mbuai watakuja kuishi humo badala ya wanadamu? Kama Mwenyezi Mungu asingalimjaalia mwanadamu jazba zimzuiazo asifanye kazi ngumu za namna hii, basi, pengine mataifa mengi sana yangeangamia kwa sababu ya majaribuo hayo. Lakini, ni fadhili ya Mwenyezi Mungu kwamba Yeye, kwa kuwalinda wanadamu, amewawekea nguvu ndani yao zinazowaokoa wengi katika maangamio.

Licha ya mtu kujitendea kama vile ilivyotajwa hapo juu kuwa ni ukatili mkubwa na ni kuharibu haki za jamii bali ni kuzuia neema za Mwenyezi Mungu, hata matokeo ya ibada za namna hii yanakuwa kwamba nafsi ya mtu inadhoofika kiasi hiki ya kuwa ndani yake haubaki uwezo wa kupambana na mawazo mabaya. Na ni jambo lililokwisha thibitika ya kuwa adhoofikapo mtu, hushindwa upesi na mawazo yake na fikira za ovyo. Basi, mara nyingi matokeo ya kudhoofisha nguvu za mwili kwa njia ya ibada za namna hii yanakuwa tu ya kwamba badala ya kuepuka dhambi binadamu anaiangukia na anaingia kinywani mwa chatu yule yule aliyetaka kumkimbia. Na wale watu wapendao kujizuilia kabisa neema alizoumba Mwenyezi Mungu kwa kutumiwa na mwanadamu, wanajinyima njia za halali za kujipatia hizo, na mara nyingi kwa kushindwa na tamaa

mbaya za kimwili wanaangukia kula haramu na kutenda haramu. Hivyo licha ya kukosa maendeleo ya kiroho hata wokovu wananyimwa.

Basi, mtu kujitia ndani ya taabu kali ndiyo kujidhulumu na kujitia maangamizoni na kupoteza nguvu zenye thamani ambazo Mwenyezi Mungu alimpa kwa fadhili zake ili apate maendeleo ya dini na dunia. Kwa hiyo, ile dini inayowafundisha wafuasi wake mafundisho ya namna hii, inawatia katika upungufu na kuitupa nafsi ya mtu katika maangamio kwa kuinyima haki bila sababu. Dini kama hii yaweza kufaa taifa mahususi tu kwa zama maalum, walakini haiwezi kufaa kwa kuongoza dunia nzima.

Kinyume na upungufu huu, baadhi za dini zingine zimepita kiasi na zimefikiria ibada hizi za kimwili kuwa zenye madhara na za upuuzi moja kwa moja. Nazo zimesema wazi wazi ya kuwa kujizoeza ibada yoyote ya kimwili ni bure na upuuzi mtupu, wala hakuna manufaa ndani yake isipokuwa hasara. Eti Mwenyezi Mungu ana haja gani ya kumtaabisha mwanadamu au kumshindisha na njaa na kiu? Na kwa sababu ya udhuru huu wao wameacha ibada zote. Lakini, jinsi zile dini, zilizohimiza kutaabisha nafsi bure kwa kujiepusha na vitu vizuri na neema, zilivyopatikana na upungufu katika kuangalia hali za nafsi, ndivyo hivyo kundi hili lilivyopita kiasi katika kuitimizia nafsi haki zake. Kwani, hakuna shaka ya kuwa wale washughulikao na kujipatia ladha za namna namna

za duniani na wakati wote wanatunza miili yao, wao miili yao inakuwa yenye kupenda starehe. Hata roho vile vile inakuwa goigoi. Pole pole nyoyo za watu kama hao zinakuwa nyeusi. Kwa maana, mwili unaungana na roho ya mwanadamu kama vile ganda la tunda linavyoungana na kiini chake. Hakuna shaka ya kuwa ganda halitakiwi lenyewe, lakini, mtakapolitenganisha ganda na kiini, basi mara moja au punde kidogo hicho kitaharibika kabisa. Hivyo, kama mwili haushirikishwi katika ibada, basi ibada kama hii inakoma upesi. Na wale watu wanaodhania kwamba ibada inahusikana na moyo tu na ya kuwa ibada ya moyo inatosha, baada ya siku kadha wananyimwa ibada ya moyo pia. Kwani katika muda kidogo tu ubichi wa roho zao unakauka na ukame unaingia. Roho inapoa kama vile kiini kilichoondolewa katika ganda. Na hata kama lisiangaliwe jambo hilo, lakini hakuna shaka ya kuwa jinsi roho ya mwanadamu ilivyo chini ya hisani ya Mwenyezi Mugnu, ndivyo hivyo mwili wake ulivyo. Basi kushughulisha roho na mwili katika ibada ndiko kunamwezesha binadamu kutimiza faradhi ya kumtolea Mwenyezi Mungu shukurani, ambayo inamlazimu kuitimiza.

Haki yenyewe ni kuwa mwili wa mwanadamu u kama farasi wa kupandwa, ambaye kwa kumpanda, mwanadamu anapitia safari ya maisha haya. Na mtu hawezi kumaliza vizuri safari yake hii ya maisha mpaka

farasi huyo awe amekuwa katika hali ya kwamba upande mmoja awe katika hali nzuri na hodari na upande mwingine ahifadhiwe na udhaifu ambao matokeo yake yanakuwa maangamio. Je, hamwoni bwana hodari anavyojitahidi kumlinda farasi wake asinone sana mpaka asifae kwa safari? Kadhalika humlinda asikonde kiasi ambacho matokeo yake yawe maangamio. Ndivyo hivyo ilivyo hali ya mwili. Bila mambo yote mawili kuangaliwa kuuhusu mwili, mwanadamu hawezi kufuzu. Upande mmoja autie mwili katika ibada ili usipate kuelekea kabisa dunia, mpaka wakati wa haja ushindwe kumtekelezea Mwenyezi Mungu amri yake. Na upande mwingine usidhoofishwe kiasi hiki kwamba usiweze kutimiza faradhi zake za kidunia na kupatwa na maradhi ya namna namna, na kuitia hasara roho kwa sababu ya hali yake ya unyonge.

Basi, ile dini isiyomfunza mwanadamu kujitendea nafsi yake namna hii, bali pengine haiijali sana na pengine inapita kiasi, hawezi kufikiriwa kuwa dini kamilifu, wala haiwezekani kwa dunia nzima kufuata dini kama hiyo. Dini ile tu yaweza kufuatwa na dunia nzima ambayo inatimiza haja zote za binadamu na kumwongoza kwenye njia ambayo kwa kuipitia mtu anaweza kumfikia Mwenyezi Mungu kwa urahisi.

Na juu ya kukiri jambo hili ya kuwa dini zote zimetoka kwa Mwenyezi Mungu, siwezi kuacha kusema ya

kwamba ikiwa kuna dini yoyote ambayo, kwa kuangalia pande zote na kufikiria tabia zote, inaeleza masala haya ya kuwa inampasa mwanadamu kujitendea nafsi yake namna gani, basi ndiyo Islam tu pekee. Ndiyo ambayo upande mmoja inawaangalia wale ambao ni wanyonge wa mwili na wenye afya mbaya, na upande wa pili inawatibu wale wanaosahau kabisa roho zao wakifikiria sana kuinenepesha miili yao. Kurani Tukufu ikieleza namna mwanadamu anavyotakiwa kujitendea nafsi yake inasema kwamba:

وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ

> Wala msijitupe kwa mikono yenu katika maangamizo (2:196).

Yaani, katika ibada, au kula na kunywa, au jitihada na bidii, au usafi na utakaso, msifuate wakati wowote njia iletayo matokeo mabaya kwa afya yenu au uhai wenu au fahamu yenu au huluka yenu.

Neno 'Tahluka' alilotumia Mwenyezi Mungu katika aya hii, maana yake ni kitendo ambacho matokeo yake yanakuwa maangamizo. Na kuna hekima kubwa katika kutumia neno hilo. 'Tahluka' maana yake ya asili ni kufanya kazi yenu kuleta matokeo mabaya. Basi, kwa kutumia neno hili Kurani Tukufu imeashiria pia ya kuwa dini ya Kiislamu haimkatazi mtu kujitia hatrini kwa kulinda dini au heshima au utamaduni. Bali, inakataza kufanya yale mambo ambayo hayatazamiwi

kuleta matokeo mazuri, ila mna hatari ya kupoteza bure maisha ya mtu au kitu kingine chenye manufaa.

Hii ni amri yenye kuhusu watu wote ambamo ndani yake mwandamu ameelezwa kanuni ya kujitendea nafsi yake. Lakini zaidi ya hayo, maelezo mengi yapatikana juu yake ndani ya Kurani Tukufu na Hadithi. Katika Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu amesema juu ya vyakula na vinywaji vya mwanadamu:

يَسْـَٔلُوْنَكَ مَاذَآ اُحِلَّ لَهُمْ ۭ قُلْ اُحِلَّ لَكُمُ الطَّيِّبٰتُ

> "Wanakuuliza wamehalalishiwa nini? Sema: Mmehalalishiwa vitu vizuri," (5:5).

Yaani, watu wanauliza kwamba wamepewa idhini ya kula vyakula gani? Uwaambie, kila kitu kisichodhuru miili yenu au fahamu zenu au huluka zenu au dini yenu, ki halaki kwa ajili yenu, hicho kitumieni bila wasiwasi.

Kadhalika anasema mahali pengine:

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُحَرِّمُوْا طَيِّبٰتِ مَآ اَحَلَّ اللّٰهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوْا ۭ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِيْنَ ۝٨٨

> Yaani, Enyi mlioamini, vitu vyovyote vizuri visivyo na madhara kwenu kwa namna yoyote vimehalalishwa; hivyo msijiharimishie nafsi zenu kamwe. (Al-Maida, 5:88)

Yaani, msiazimie nafsini mwenu kwamba tunajiharimishia kitu fulani kwa kuitiisha nafsi, ingawa kitu hicho hakina madhara kwa afya ya mwili, na usalama wa fahamu, na usawa wa huluka na ulinzi wa

dini. Na zaidi ya hayo, kumbukeni jambo hili vile vile ya kuwa kama upande mmoja hamna ruhusa ya kujiharimishia vitu hivyo, basi upande mwingine hamna ruhusa pia ya kuwa mjitie tu katika kula na kunywa na mkasahau wajibu wenu mwingine. Mkifanya hivyo, basi kitendo chenu hicho kitakuwa kimeruka mipaka, na Mwenyezi mungu hapendi kamwe urukaji wa mipaka na kuelekea upande mmoja tu.

Fikirini juu ya aya hii ya kwamba kuhusu kula na kunywa namna gani imekatazwa, upande mmoja, kunyima nafsi vitu vizuri na vyema bila sababu, na upande mwingine kuzama katika kulea mwili tu peke yake pia kumekatazwa.

Je, si maagizo hayo yanayoafikiana na kila tabia, na kila nchi, na kila zama na kila mtu mnyonge na mwenye nguvu? Tena, je, iko dini, ghairi ya Islam, inayo-mwongoza mtu namna hii? Kama haiku, basi, je, haithibitiki kwa ukamilifu ya kuwa islam tu ndiyo dini iwezayo sasa kumfikisha mtu kwa Mwenyezi Mungu, na ambayo maagizo yake yaweza kuwaongoza wanadamu wote?

Zaidi ya aya iliyotajwa hapo juu, kuna aya nyingine vile vile katika Kurani Tukufu inayohusu kula na kunywa nayo ni hii:

كُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴿٣١﴾

"Kuleni na kunyweni wala msipite kiasi", (7:32)

Yaani, isiwe ya kwamba mjitolee wakfu maisha yenu yote kwa kutumia vyakula vizuri na vinywaji baridi tu peke yake, bali, sawa na haja, tumieni kitu chochote kizuri bila wasiwasi. Kuhusu vyakula na vinywaji na vitu vingine vya mapambo na starehe anavyovitumia mwanadamu, Mwenyezi Mungu anasema:

قُلْ مَنْ حَرَّمَ زِينَةَ اللّٰهِ الَّتِيٓ اَخْرَجَ لِعِبَادِهٖ وَالطَّيِّبٰتِ مِنَ الرِّزْقِ

> Sema: Ni nani aliyeharimisha mapambo ya Mwenyezi Mungu ambayo Amewatolea watu wake, na vitu vizuri vya riziki? (7:33)

Muradi wake ni kwamba Mwenyezi Mungu ameviumba vitu fulani kwa mapambo, basi, ni nani tena anayeweza kukataza ya kuwa asivitumie yeyote. Kama kuvitumia hivyo hakungejuzu, basi kwa nini, tena, Mwenyezi Mungu akaviumba?

Kadhalika, Mtume[saw] amesisitiza juu ya kufanya ibada ya nafali kadri nafsi inayoridhia; na nafsi ichokapo, basi iacheni mara moja. Kumhusu Mtume[saw] imesimuliwa ya kuwa sfari moja yeye aliingia msiktini na humo akaona kamba moja ikining'inia. Akauliza, ya nini hii? Watu wakajibu ya kwamba mama wa waaminio, bi Zainab[ra], ameining'iniza kwa sababu anaposhughulika katika sala, basi, kama akipata usingizi sana anaitegemea kamba hii. Mtume[saw] akasema kamba hii iondolewe sasa hivi; ibada ya namna hii hairuhusiwi. Kadhalika kuhusu saumu, imesimuliwa na bwana Abdullah bin Umar[ra] kwamba

Mtume[saw] alipata habari kuwa yeye (Bwana Abdullha bin Umar[ra]) amesema kwamba atafunga saumu siku zote. Basi, Mtume[saw] akamwita na kumwambia, hiyo si sawa. Lakini yeye alipokazania mno alimruhusu kufunga siku moja na kuacha kesho yake. Na (Bwana Abdullah) aliposema mimi ninao uwezo zaidi wa kufunga saumu, yaani, naweza kuvumilia zaidi, akasema hakuna saumu bora kuliko (kufunga) kiasi hiki. Yaani, ikiwa mtu atafunga zaidi ya kadri hiyo, afya yake itaharibika na mtokeo yake hayatakuwa mema. Basi, mwishowe Mtume[saw] akamwaga akisema: "Ee Abdullahi, mwili wako pia una haki juu yako, na macho yako vile vile yana haki kwako, na mkeo pia ana haki juu yako".

Kadhalika, juu ya kupoteza baadhi ya sehemu za mwili, imesimuliwa katika Hadithi ya kwamba baadhi ya masahaba walipofanya shauri la kujihasi, ili wakae makapera maisha yote, Mtume[saw] aliwakataza. Mtume[saw] hata hakupenda fikira ya kutooa, Amesema:

لَا رَهْبَانِيَّةَ فِي الْإِسْلَامِ

"Hakuna uruhubani katika Uislamu."

Yaani, Uislamu hauruhusu wanaume na wanawake kukaa bila kuoa na kuolewa maisha mazima kama wafanyavyo Wakristo.

Kwa merejeo yote yaliyopita nadhani mmekwisha fahamu namna Uislamu ulivyotoa maagizo kamili na

matimilifu kuhusu sehemu hii ya kuwahurumia viubme vya Mwenyezi Mungu na namna gani Waislamu wamelekezwa kwenye njia ya katikati kwa kujiepusha na kuzidisha na kupunguza sana! Amri hizi zaweza kufanya kazi katika kila zama na kila nchi. Ikiwa upande mmoja dini ya Kiislamu imeamrisha mwili utiwe katika jitihada na ibada, ili kuushirikisha mwili wa binadamu katika hali ya roho, bali kuizidishia roho nguvu, upande mwingine, imeulea na imeagiza kuutimizia haja zake. Na Uislamu umeangalia sana afya ya binadamu hata katika ibada hizi fupi walizolazimishwa Waislamu, urahisi mwingi umewekwa katia hali ya kuugua au safari ili zisiwe ngumu kwa mtu wala zisiharibu nguvu za asili za mtu yeyote.

Basi, kuhusu sehemu hii pia ya sheria, Islam tu ndiyo dini inayotoa maagizo kamili ambayo watu wote wa dunia nzima wanaweza kuyafuata.

## Kuwatndea Wanadamu wengine

Sehemu ya pili kuhusu kuvihurumia viumbe vyote vya Mwenyezi Mungu huwa ni yale mafundisho ambayo dini inawatolea wafuasi wake juu ya kuwatendea wanadamu wengine. Basi, baada ya kumaliza sehemu ya kwanza, tutaeleza hii sehemu ili ijulikane ya kuwa Uislamu unazishinda dini zingine katika jambo hili vile vile.

Lakini, kabla ya kueleza sehemu hii kwa kirefu yatupasa kueleza kwanza kwa kifupi maagizo yaliyomo ndani ya

Kurani Tukufu kuhusu kuwatendea wanadamu wote kwa jumla. Mwenyezi Mungu anasema katika Kurani Tukufu:

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنكَرِ وَالْبَغْيِ ۚ
يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٩١﴾

> Mwenyezi Mungu anawaamuruni uadilifu na hisani na kuwapa watu kama uwapavyo ndugu; na anakataza upujufu na uovu na uasi. Yeye anawanasihini ili mpate kufahamu, (16:91).

Katika aya hii Mwenyezi Mungu amemwamrisha kila Mwislamu kufanya mambo matatu na kumkataza mengine matatu. Ndio kusema kuwa kulingana na kila amri kuna katazo moja: na kwa kila wema ulioamrishwa ufanywe, umeelezwa uovu mmoja vile vile uliolingana nao kwamba mjiepushe nao.

Kipago cha kwanza ambacho mumini ameamrishwa kukikanyaga ni cha uadilifu, yaani asimnyime yeyote haki. Ikiwa ameajiriwa na mtu, basi afanye kazi yake kwa uaminifu, na sawa na mshahara anaopata afanye kazi walivyyopatana. Akiwa kibarua, basi atumie wakati wake kwa bidii katika kazi ya mtu aliyemwandika. lkiwa anadaiwa, basi alipe. Na ikiwa anamwia mwingine haki yoyote, basi aitoe kwa uaminifu. Ilmuradi, afanye adili katika kila kitendo chake wala asimnyime yeyote haki yake. Aitoe sawasawa. Baada ya hayo Amesema (Mwenyezi Mungu) ya kuwa mumini akiisha panda kipago cha adili, basi hapo anatakiwa kukanyaga kipago

cha 'Hisani'. Yaani, licha ya kumtolea kila mtu haki zake sawasawa, hata amwongezee kwa sababu ya hali yake ya imani kupata kuendelea. Na kule kuwafanyia watu adili liwe ni jambo dogo tu la kawaida kwake, na sasa afikirie tu kwamba kwa njia gani anaweza kuwafaidisha watu kwa uwezo wake, nguvu yake, utajiri wake, mali zake, heshima yake na uwajihi wake. Na afikiapo daraja hilo pia, ndipo atakiwapo Mwislamu kuinuka juu zaidi mpaka kufanya hisani vile vile kuwe ni jambo dogo tu machoni mwake. Bali ajipatie daraja la "*Itai dhil kurba*" ambalo ndilo daraja kubwa mno kuliko hisani.

Tofauti kati ya "*Hisani*" na "*Itai dhil kurba*", ni kwamba mtu mmoja anamfanyia mwingine hisani katika hali fulani. Yaani, alipomwona fulani katika shida akamhurumia na kumfanyia hisani. Au mtu anamfanyia hisani mwenzake kwa kukumbuka wema aliomtendea zamani. Ilmuradi, hisani ya kawaida huhimizwa na rehema na huruma. Lakini, utoaji kama ule wa kuwapa jamaa si matokeo ya rehema na huruma. Mama humtumikia mtoto wake na kudekewa naye si kwa sababu anamwona katika hali mbaya au katika msiba. Bali, kwa kuwa yu ini lake, na ni mwanaye. Mara nyingi hutokea ya kwamba watoto wanakuwa matajiri ambapo wazazi wanakuwa maskini. Lakini wazazi wanaendelea kuwatendea watoto wao sawa na uwezo wao kidogo kama wazazi waliotajirika wawatendeavyo watoto wao

sawa na utajiri wao. Basi, wazazi hawasaidii watoto wao kwa sababu ya matamanio ya kulipwa au kwa kulipa hisani waliyofanyiwa zamani, wala si kwa sababu ya jazba ya huruma kwa kuwaona watoto wao katika shida. Bali kutenda kwao huku kumeepukana na hayo yote; waila sababu yake huwa upendo tu. Basi, "*Itai dhil kurba*", yaani kutoa kama jamaa wanavyotoleana, huwa hisani ya daraja ya juu kuliko hisani ya kawaida. Kwenye hilo Mwenyezi Mungu anawaita Waislamu na anasema kuwa haimpasi mumini kubaki katika daraja ya hisani tu, bali inampasa kuendelea mbele na kuwapenda wote kama baba mkarimu na mama mwenye upendo wampendavyo mtoto wao. Kutenda huku kwa wema kusifanyike kwa kubagua utajiri na umaskini, na huu mwungano usiwe kwa sababu ya upendo wa muda tu.

Kadhalika, pamoja na kujipatia wema huu wa namna tatu, yeye ajiepushe na maovu matatu. Yaani, aache yale maovu yamhusuyo dhati yake na aepuke na yale vile vile ambayo japo yamhusu dhati yake, lakini ni ya namna ambayo watu wengine pia wanayajua na kuyachukia. Vile vile aachilie mbali yale maovu ambayo ni sababu ya kuwanyima wengine haki zao, au yanayoharibu taratibu za serikali. Kwa kuunganisha maamrisho hayo mawili, Uislamu umekamilisha madaraja yote ya kuwahurumia viumbe. Kwa maana, huruma huwa ya namna mbili tu. Kwanza, kutenda wema, pili, kuondoa shari. Katika aya

hii namna zote hizo mbili zimeelezwa kwa ukamilifu. Mwislamu anatakiwa kuwatendea wema wanadamu kiasi hiki ya kwamba kwa kuendelea mbele tokea 'adili' yeye afikie hadi ya kuwa awatendee kwa upendo hasa na awafanyie hisani bila ya kubagua kama wazazi wamfanyiavyo mwana. Na vile vile inampasa kujitenga na maovu na maasi ya hatari na shari kubwa kubwa ili afikie hatua ya kujiepusha na yale maovu yafichikayo nafsini mwake tu, kwani, inawezekana mtu mwingine kupata madhara kwa hayo kwa njia isiyojulikana. Basi, madaraja yote ya pande zote mbili za kuwahurumia viumbe wa Mwenyezi Mungu kuwafanyia wema na kuwaondolea shari yameelezwa katika aya hii. Na zaidi ya hayo hakuna daraja yoyote ya kuwahurumia viumbe vya Mwenyezi Mungu anayoweza mwanadamu kupata, wala hakuna ovu jingine jepesi analoweza mtu kuliepuka. Kwa hiyo kuhusu kuwahurumia viumbe wa Mwenyezi Mungu, hakuna dini nyingine inayoweza kuleta agizo kubwa kuliko hili. Agizo lililo la daraja ya juu kabisa, Uislamu umekwisha simama pale, na hakuna nafasi ya mtu kuendelea mbele. Licha ya kuleta maagizo bora twaweza kudai ya kuwa hata hakuna dini iwezayo kuleta maagizo yaliyo sawa na haya.

Baada ya kueleza maagizo yaliyotolewa na Uislamu kwa kifupi juu ya kuwahurumia viumbe vya Mwenyezi Mungu, sasa naeleza yale maagizo ambayo dini ya

Kiislamu inawatolea wafuasi wake kwa kirefu kuhusu kuwahurumia viumbe vya Mwenyezi Mungu. Kwanza kabisa naeleza yale mafundisho yanayotolewa na Uislamu kwa jamaa wa karibu.

## Uhusiano kwa Wazazi

Uhusiano mkubwa kabisa katika maisha ya kidunia huwa wa mtu kwa wazazi wake miongoni mwa wanadamu wote. Kwani Mwenyezi Mungu amewafanya wazazi kuwa njia ya kumleta mtu duniani. Jinsi mapenzi ya wazazi yanavyokuwa halisi na bila uchoyo, mfano wake unapatikana kidogo tu katika dunia. Wanamtunza mtoto asipojijua mwenyewe, wala hawezi kujipangia mpango kwa kusimamisha maisha yake. Katika hali kama hii taabu wanazopata wazazi katika kumlea mtoto, wazazi tu wanaweza kuzijua na mtu mwingine hawezi hata kuziwazia. Ndiyo sababu mtoto hana uwezo wa kulipa hata sehemu ya mia moja ya mapenzi ambayo kwayo wazazi wanamtunza yeye. Watapatikana watoto wachache sana ambao wangeweza kutoa malipo sawasawa ya hisani waliyowafanyia wazazi wao. Ndiyo maana, Uislamu umetoa amri kali ya kuwatii. Ndani ya Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu asema:

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوٓا۟ إِلَّآ إِيَّاهُ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَٰنًا ۚ إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِندَكَ ٱلْكِبَرَ أَحَدُهُمَآ أَوْ
كِلَاهُمَا فَلَا تَقُل لَّهُمَآ أُفٍّ وَلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُل لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ وَٱخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ ٱلذُّلِّ مِنَ
ٱلرَّحْمَةِ وَقُل رَّبِّ ٱرْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِى صَغِيرًا ﴿٢٤﴾

Yaani, Mola wako Ameagiza kuwa msimwabudu yeyote ila Yeye tu, na kufanya wema kwa wazazi:

> kama mmoja wao akifikia uzee pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie hata Akh! Wala usiwakemee, na useme nao kwa msemo wa heshima. Na uwainikie bawa la unyenyekevu kwa huruma. Na useme: Mola wangu, Uwarehemu kama walivyonilea katika utoto, (17:24-25).

Hayo ndiyo maagizo yasiyo na mfano, inayotoa Islam kuhusu wazazi. Kuna dini gani nyingine duniani inayoweza kutoa maagizo yaliyo mfano wa hayo? Hakuna shaka, dini zote zina mambo mengine mazuri; na kwa kuwa hizo zimepelekwa na Mwenyezi Mungu, hivyo yapo mambo mengi ya kikweli ndani yao. Lakini, maagizo kamili, ambayo ndani yake hakuna kupita kiasi kuhusu jambo fulani wala kutokujali hilo, unayotoa Uislamu hayapatikani katika dini nyingine iwayo yote ile. Katika aya moja tu peke yake Uislamu umeeleza kwanza ya kuwa ibada inapaswa kufanywa kwa Mwenyezi Mungu tu pekee na kuwa hisani ya wazazi si kitu mbele yake. Basi, ninyi msifuate ile dini inayopita kiasi katika kuangalia haki za wazazi hata inahalalisha kuwasujudia na kuwaabudu. Hakika, jambo hili limepita kiasi, na kwalo Ameondolewa heshima Yule Mhisani wa kweli aliye Mwumba wa ile hisani ambayo wazazi wanamfanyia mtu.

Jambo la pili lililoelezwa katika aya hii ni kwamba ingawa haipasi kuwaabudu wazazi, lakini inalazimu

kuwafanyia hisani. Hayo ndiyo maagizo ambayo mbele yake haiwezi kusimama dini yoyote. Dini zingine zinasema tu ya kuwa: Uwafanyie wema wazazi na kuwatumikia. Lakini, Islam haisemi tu ya kwamba uwatendee wema, bali yasema ujitahidi kuwafanyia hisani. Na hisani ni utumishi au neema iliyozidi huduma au neema ya mwingine. Ikiwa mtumishi anafanya kazi ya mtu fulani na huyo mtu baadaye anamtolea haki yake basi huyo haitwi ni mfadhili wake. Mfadhili huitwa yule amlipaye zaidi ya haki yake. Basi, Islam ilipoagiza kuwatendea wazazi, haikusema ya kwamba uwatendee wema. Kwani, yawezekana kuwa mtu awafanyie wema wazazi wake, lakini kuwatendea huku kusifikie hata nusu ya kile kiasi cha wema walichomfanyia wazazi. Hapo, kutenda huku kwa mtu huyo kutaitwa wema lakini yeye hawezi kuitwa mfadhili wao. Anaweza mtu kuitwa mfadhili hapo tu awatendeapo wazazi kwa mapenzi zaidi kuliko walivyomtendea yeye. Tazameni, basi, kwa kuangalia huruma ya wazazi, Uislamu umetoa mafundisho matukufu namna gani juu ya wazazi. Je, iko dini nyingine vile vile iliyoeleza kuwatendea wazazi kwa njia hii? Upande mmoja kupita kiasi kumekatazwa na upande mwingine kuwapunguzia haki kumepigwa marufuku. Upande mmoja imeangaliwa haki ya Mwenyezi Mungu kwa kukataza kuwaabudu wazazi, na upande mwingine zimekanushwa zile dini ziangaliazo haki za mke lakini haziagizi lolote juu ya wazazi. Dini

hizo zinamstahilisha mke tu kuangaliwa baada ya ndoa. Islam inasema ya kuwa wazazi wakifikia uzee, basi msiwaambie "Akh, hatupendi kitendo chenu fulani". Sharti ya uzee imewekwa kwa sababu hizi: Kwanza, wazazi wanapokuwa wanaweza kufanya kazi hawawabebeshi watoto wao mizigo. Pili, mtu awapo mzee, huwa mwepesi wa kukasirika kwa sababu ya kutokuweza kutumia mikono na miguu, na kwa sababu ya magonjwa ya namna mbalimbali na unyonge. Basi, hata katika hali wanapokuwa wasumbufu na wakali, msidhihirishe ninyi hasira juu ya jambo lao lolote ingawa mambo yao yaonekane hayavumiliki. Bali, mkiweza kulitimiza, litimizeni. Na kama hamwezi, basi waambieni kwa upole sana kwamba jambo hilo halimo katika uwezo wenu. Na mnapozungumza nao, basi zungumzeni kwa adabu sana, na mlainike kwao sana kana kwamba mmejilaza mbele yao kwa kuwahurumia. Si hayo tu, bali mdumu katika kuwaombea kuwa upungufu upatikanao katika kuwatumikia wazazi, Mwenyezi Mungu awalipe kutoka kwake mwenyewe.

Huku ndiko kutenda wema ambako Islam imewaamrisha watoto wanapokuwa hai. Lakini ikiwa mtu anafariki ilhali wazazi wake wako hai, hapo vile vile Islam haikuwasahau wazazi, wala kwa kuwaangalia hao haikuwasahau jamaa wengine. Haikuagiza dini ya Kiislamu kama dini zingine, ya kuwa mali zote za wana

wapewe wazazi, kwani kwa njia hii baadhi ya jamaa wengine ambao nao wanastahili kuhurumiwa hunyimwa haki. Kwa mfano, ikiwa ameacha mkewe na watoto wachanga, wao hawatabaki na chochote chini ya amri hiyo. Wala Islam haikuagiza kuwa wazazi wanyimwe kabisa, kama yalivyo mafundisho ya baadhi ya dini. Bali, kinyume na mafundisho hayo ya namna mbili Islam imechagua njia ya katikati, nayo ni kwamba imewawekea wazazi sehemu katika urithi wa marehemu. Yaani, kama wamebaki watoto wake, basi wazazi watapata sehemu ya sita kila mmoja. Na kama hakuna watoto, basi, theluthi ya mali ataipata mama mzazi, na yaliyo baki atayapata baba. Lakini, watapewa baada ya mume au mke kutolewa sehemu yake.

## Wazazi Kuwatendea Watoto wao

Amri juu ya watoto kuwatendea wazazi tumekwisha eleza hapo juu. Sasa twaeleza jinsi wazazi walivyoagizwa kuwatendea watoto wao. Hakuna shaka ya kuwa kuwapenda watoto ndiyo tabia ya asili ya wazazi, na inaonekana hawana haja ya kuamrishwa wawatendee wema watoto wao. Lakini historia ya ulimwengu yatuambia sivyo hivyo. Bali, juu ya mapenzi yaliyomo ndani ya tabia ya asili ya wazazi kwa watoto wao, ipo haja kwa sababu kadha ya kwamba wazazi vile vile waamrishwe wawatendee watoto wao namna gani. Na historia ya dini mbalimbali inatuarifu ya kwamba kwa

sababu ya kutokuwapo maagizo haya wafuasi wa dini hizo wamekabiliwa na mashaka makubwa. Juu ya mambo yote yale — isipokuwa jambo la urithi, maana linahitajiwa katika kila nyumba — dini zote zimenyamaa kimya kabisa zisieleze wazazi wanapaswa kuwatendea watoto wao namna gani. Lakini, Islam, ikiwa dini timilifu na ya mwisho na imekuja kwa wanadamu wote, haina upungufu huu. Kwani, imefika katika zama ambamo hali ya binadamu ilihitaji kupata sheria iliyokamilika kwa kila jiha ambayo inaangalia pande zote za mambo yanayowahusu wanadamu wanavyotendeana wao kwa wao. Dini zilizokuja kabla ya Islam zilikuwa na haja ya maagizo kiasi tu ya kutosheleza mahitaji ya wakati ule tu, na kwamba kwa njia hii wanadamu watayarishwe kwa kupokea Sheria kamili iliyokadiriwa tangu azali kwa mwongozo wa binadamu.

## Kuwaua Watoto

Katika nchi mbalimbali kulikuwa na desturi ya kuwaua watoto kwa sababu fulani fulani. Baadhi ya watu walikuwa wakiua binti zao, eti kwa sababu wataolewa katika majumba mengine na hii itakuwa ni fedheha kwao. Wengine waliwaua mabinti kwa kuhofia isije watakapobalehe wakaangukia dhambi na wakawa sababu ya kuwafedhehesha. Wengine walikuwa wanaharibu mimba yao kwa sababu ya umaskini wakifikiria kwamba nani atawalisha watoto! Katika siku

hizi ambapo elimu imekuwa taabu, watu wengi wa Ulaya, Amerika na Asia wanajitafutia njia za kuzuia kizazi. Hii pia ni namna mojawapo ya kuharibu mimba. Wao waulizwapo, kwa nini wanafanya hivyo, wanasema siku hizi elimu ya shule ni ghali sana, na watoto wakiwa wengi itakuwa taabu kuwaelimisha. Islam inachukia sana kitendo hiki na inasema:

وَإِذَا الْمَوْءُدَةُ سُئِلَتْ ۝ بِأَيِّ ذَنْبٍ قُتِلَتْ ۝

"Na msichana aliyezikwa hai atakapoulizwa juu yake, kwa kosa gani aliuawa," (81:9-10).

Tena yasema:

وَلَا تَقْتُلُوٓا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَاقٍ ۖ نَحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ ۚ إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا ۝

"Wala msiwaue watoto wenu kwa kuhofia umaskini. Sisi ndio Tutawaruzuku wao na ninyi pia. Hakika kuwaua ni hatia kubwa", (17:32).

Yaani, msiwaue watoto wenu kwa kuhofia kwamba mali yenu itatumika kwa kuwalea na kuwaelimisha na kuwalisha na kuwanywesha. Kwani, chochote mpatacho mnapewa kutoka katika hazina yetu, nasi tutawapa wao vile vile. Kisha ili kuondolea mbali shaka kwamba je, kuwaua watoto kumekatazwa kwa sababu hii tu ya kuhofia mali kuangamia peke yake au kwa sababu nyinginezo vile vile, Kurani Tukufu inaongeza kusema:

إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا

"Hakika kuwaua ni dhambi kubwa kabisa".

Yaani, siyo tu kwamba kuwaua kwa sababu ya hofu ya mali kuangamia ndiyo dhambi, bali sababu ya asili ya katazo hili ni kwamba kuwaua kwenyewe, hata kwa sababu gani, ni dhambi na tendo ovu, na sababu iliyoelezwa hapo juu ni kwa njia ya mfano tu.

Hayo ndiyo maagizo ya Islam kuhusu uuaji wa watoto. Baadaye yaja mafundisho yaliyo na amri zinazohusu kulea na kuwaelimisha watoto. Agizo la kwanza lahusu usimamizi wao. Mwenyezi Mungu Anaamuru ndani ya Kurani Tukufu kwamba baba ndiye mlinzi wa watoto wake. Na hivyo watoto wamelindwa katika maangamio wanayokabili ambapo, pengine wazazi wagombanapo, baadhi ya baba wanajizuia wasitoe matumizi ya watoto kwa mama waliomchukia. Sawa na agizo hili, baba aridhike asiridhike, serikali itamshurutisha awatolee watoto wake matumizi sawa na njia zake za uchumi mpaka watoto kubalehe.

Isitoshe, Uislamu unakazania mno kuhusu ulezi wa watoto vile vile. Katika Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Anasema:

يَآاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا قُوْٓا اَنْفُسَكُمْ وَ اَهْلِيْكُمْ نَارًا

> Yaani, Enyi waaminio, jiokoeni nafsi zenu na ahali zenu (mke na watoto) katika moto. (66:7)

Yaani, waelimisheni na kuwalea vizuri, wala msiwaache wayueyue na kubaki katika hali ya ujinga, wakampe kisogo hata Mwenyezi Mungu, na hatimaye wakaangamia.

Kadhalika, kuhusu ulezi wa watoto imeamrishwa katika Hadithi ya Mtume[saw] kuwa "Waheshimuni watoto wenu, wala msiwatendee kwa namna ambayo iwafanye kuwa wenye tabia mbaya. Tena, amesema Mtume[saw] ya kwamba kuwaelimisha watoto na kuwafunza hekima ni bora kuliko sadaka. Na hii ni kweli kabisa, maana anayewahurumia watu wengine tu na anasahau kulea watoto wake, wema wake utakoma palepale atakapoondoka duniani. Lakini, yule mtu awaelimishaye watoto wake na kuwafunza, yeye huacha wazi mlango wa kutenda wema hata baada ya yeye kufariki. Vilevile imekatazwa kuwapiga watoto. Imeagizwa si sawa kuwatesa na kuwasumbua watoto. Hekima yake ndiyo hii ya kuwa kupiga na kutesa siku zote huharibu mienendo na kuichafua. Na mtu anakuwa hafai tena kitu katika maisha ya baadaye. Lakini kwa kuwa katika kuwalea watoto pengine inatokea haja ya kuwachapa pia, basi, imetolewa amri ya kuwa dharura na shida kali ikitokea, wasipigwe usoni; bali wapigwe sehemu ambayo pigo halileti hasara mwilini mwao.

Tena, ili kudumisha mapenzi ya ndugu, imeamrishwa ya kuwa yawapasa wazazi kuwatendea wana na mabinti kwa usawa; haifai kuwapendelea baadhi tu kati yao; kwa maana, matokeo yake huwa fii na ugomvi. Imeandikwa kuwa mtu mmoja alimjia Mtume[saw] na akasema: Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu, mimi nimempa

mwanangu fulani mtumwa mmoja, basi wewe uwe shahidi. Mtume,[saw] akasema, je, umewapa wanao wote mtumwa mmoja mmoja? Akanena, hapana. Akamwuliza, je, wapenda wote hao wawe wema namna moja? Akajibu, ndiyo. Akasema., unatakaje, basi, kumpendelea mmoja tu kwa kumpa zawadi? Hii haijuzu. Umpe kila mmoja wao au ujirudishie mtumwa kwa mwana yule. Basi, kwa njia hii akamwambia. kwamba ikiwa utampendelea mmoja kuliko wengine, basi, matokeo yake yatakuwa kwamba watamfanyia bughudha na mwishowe watakuwa maadui zake na kuangukia dhambi. Basi, kama baba yeyote hataki watoto wake waangukie dhambi na kufuata njia ya kuwapeleka mbali na Mwenyezi Mungu, anatengenezaje, basi, kwa mikono yeke, njia ya kuwafanya baadhi ya watoto wake kuwa wenye dbambi? Linganisheni maagizo hayo na desturi wanayoshika watu fulani kwa kuwatendea watoto wao ya kwamba wanamrithisha mmoja wao tu na kuwanyima wengine wote. ltajulikana kuwa dini ya Kiislamu imeeleza kwa uwazi mno masaala magumu haya ili watu wasikwae na kuangamia. Aidha, Islam imeagiza pia ya kwamba hata baada ya mtu kufariki, yeye hawezi kumwongezea mwanaye yeyote mali.

Zaidi ya maamrisho haya, Uislamu, kwa kujua hali mbaya sana ya wanawake, umetoa amri maalum juu ya mabinti. Mtume[saw], amesema ya kuwa anayejaaliwa

mabinti wawili naye akawaangalia vizuri, basi hao watakuwa sababu ya kumwokoa katika moto.

Katika amri hizi zote, mtu anaweza kujua kuwa upande huu wa kuvihurumia viumbe vya Mwenyezi Mungu, ambao dini zingine zimeuacha kabisa au zimetoa maagizo mapungufu juu yake, dini ya Kiislamu imeeleza namna gani kwa ukamilifu, na namna gani imewaongoza wazazi kwenye njia ambayo kwa kuifuata wanaweza kujiokoa na kuokoa watoto wao pia katika maangamizo. Je, ipo dini nyingine iliyotoa maagizo kwa kirefu kuhusu watoto? Kama haiko, basi, dini yoyote ina haki gani ya kudai kusuluhisha dunia? Hizo dini zimekwisha maliza zama zao. Hizo pia zimewafaidisha watu katika nyakati zao; lakini, baada ya kuja kwa dini hii iliyokamilika, sasa hazina haja!

## Maagizo Kuhusu Ndugu

Pamoja na wazazi na watoto, dini ya Kiislamu haikuwasahau ndugu wa kike na kiume, na imeagiza kuwatendea hao vile vile wema. Na imekamilisha kutendea huku kwa kuwafanya warithi wa mali ya ndugu kama wazazi na watoto hawapo.

## Maagizo Kuhusu Mke

Ijapokuwa wafuasi wa dini mbalimbali wanadai katika zama hizi za maendeleo ya elimu ya kuwa dini yao inaeleza na kulinda haki za wanawake zaidi kuliko dini

nyingine zote, lakini madai haya hayastahili kuangaliwa. Kwani hakuna mtu aelezaye haki za wanawake kutoka katika vitabu vya dini yake. Bali sawa na hali ya utamauuni wa zama hizi, madai ya mtu binafsi yanaletwa, ilhali tendo la mtu au kaumu fulani haliistahilishi dini yake kusifiwa mpaka maagizo hayo yaletwe na dini yenyewe. Na twaona ya kuwa dini nyingine zote, ghairi ya Islam, kwa kuwa zilikuwa kwa zama na kaumu maalumu, zimenyamaa kimya kuhusu hali ya wanawake, japo zina mambo mamia mengine mazuri. Hata Ukristo, dini iliyo karibu sana na Uislamu, pia hauna maelezo mapana juu ya wanawake. Mwendo wa Wazungu hauwezi kuwa sababu ya fahari kwa Ukristo. Maana haukupatikana kwa sababu ya maagizo ya Ukristo, bali ni matokeo ya elimu kuendelea mbele na kusuhubiana na Uislamu. Naam, Islam tu ndiyo dini iliyoangalia haki ya wanawake na kuwainua baada ya kudhulumiwa sana. Huruma yake haikuhusiana na kundi moja tu la watu. Maagizo yanayohusu mama, binti na dada yametolewa na Uislamu, nasi tumekwisha yaeleza hapo juu. Sasa twaeleza mafundisho yaliyoagizwa na Uislamu kuhusu mke.

Miongoni mwa dini nyingine, ziko dini nyingi zisizogusa hata madhumuni haya. Na zile zilizoyagusa kidogo, basi maagizo yake ni mapungufu sana wala hayakupevuka. Hayo maagizo huenda yalitosha kwa kuwaokoa

wanawake katika baadhi ya dhuluma kali miaka mamia kabla ya leo ambapo hali ya elimu na ustaarabu ilikuwa mbaya mno. Lakini, sasa, ambapo dunia imepuliziwa roho ya uhai, haiwezekani kuangalia haki za mabibi kwa kufuata maagizo hayo ya zamani. Maagizo yaliyotolewa na Uislamu tu pekee ndiyo yaliyokamilika na kiasi cha kuwapatia mabibi haki zao.

Fundisho la kwanza lililotolewa na Uislamu kwa kuinua wanawake mara moja toka hali ya chini mpaka kuwapa daraja sawa na wanaume ni lile ambalo lasema kuwa wanawake na wanaume wanafanana na ni jinsi moja tu. Hili limewastahilisha kupata haki sawasawa. Katika Kurnai Tukufu Mwenyezi Mungu asema:

وَاللّٰهُ جَعَلَ لَكُمْ مِّنْ اَنْفُسِكُمْ اَزْوَاجًا

"Na Mwenyezi Mungu Amewajaalieni wake katika jinsi yenu", (16:73).

Basi, haiwapaseni kuwadharau na kuwatendea kwa ukali kwa kuwafikiria kuwa viumbe duni. Zaidi ya hayo limo agizo katika Kurani Tukufu kuhusu haki za wanaume na wanawake, kwamba:

وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِيْ عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوْفِ ۖ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ ۗ

Yaani, nao (wanawake) wanayo haki sawa na ile iliyo juu yao kwa sheria; na wanaume wana daraja moja zaidi kuliko wao katika usimamizi wa mambo. (2:228)

Yaani, shauri la mwisho katika mambo ya nyumbani li mkononi mwa mwanamume. Na hili ndilo agizo lililoondoa dhuluma inayofanywa kuhusu haki za wanawake.

Baadhi ya watu wanawaacha wake zao kama walioangikwa na hawawatendei wema. Juu yao imetolewa amri hii:

وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَآ ءَاتَيْتُمُوهُنَّ

"Wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa", (4: 20).

Tena imeagiza:

وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ

"Na kaeni nao kwa wema", (4:20).

Kisha, ili kukamilisha haki za wanawake, Islam inawafanya warithi wa sehemu ya nane ya mali iliyoachwa na waume zao kama wameacha watoto; na kama hawakuacha watoto, basi watapata robo.

Tena mali wanayomiliki wanawake ndiyo yao kabisa; siyo ya wazazi au ya waume zao.

Zaidi ya maagizo ya Kurani Tukufu, Mtume[saw] pia amesimamisha haki za wanawake kwa kukazania sana kwa matendo yake na maamrisho yake, mpaka amepata kusema:

خَيْرُكُمْ خَيْرُكُمْ لِأَهْلِهِ

"Mbora wenu ndiye amtendeaye wema mkewe."

Kadhalika, amesema: Enyi Waislamu , kubalini shauri langu kuwahusu wanawake, ya kwamba watendeeni kwa wema. Hamna haki ya kuwatendea wake zenu ila kwa wema tu, isipokuwa watendapo ovu lililo dhahiri wanalochukia watu wote. Kama wakitenda ovu la namna hii, basi jitengeni nao kwa siku kadha. Kama wakijisawazisha ni vizuri, waila waadhibuni kwa kuwachapa, lakini, msiwatie alama mwilini mwao kwa adhabu hiyo.

Kama Uislamu ulivyoweka haki za mke juu ya mume. Ndivyo hivyo ulivyoweka juu ya mke haki za mumewe vile vile. Mke ameamrishwa kumtolea mumewe amana yake sawasawa, na kuangalia starehe na raha ya mumewe, na ashirikiane naye katika wakati wa taabu. Awalee watoto wake. Wala asiwe mtovu wa shukurani kwake.

Basi, haikufanywa hivi kwamba zimetajwa haki za wanaume tu na hazikutajwa haki za wanawake; au kwamba zimelezwa haki za wanawake tu na hazikutajwa haki za wanaume; au zimetajwa haki zao wote, lakini haki za hawa zimezidishwa na za wale zimepuguzwa; la. Bali zimeelezwa zilivyofaa sana haki zote za wanaume na wanawake kwa kuangalia pande zote. Hivyo, ule mwungano mkuu ulio mzizi wa maendeleo yote ya binadamu umejengwa imara juu ya mwamba

madhubuti, hata imekuwa kwamba hakuna kimbunga au dhoruba linaloweza kuutikisisha.

## Kuwatendea Jamaa Wengine wa Karibu

Pamoja na hao jamaa wa karibu sana ambao haki zao zimeelezwa hapo juu, dini ya Kiislamu haikuwasahau jamaa wengine vile vile. Ndani ya Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu anasema:

فَآتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ

"Basi, mpe jamaa wa karibu haki yake."(30:39).

Katika agizo hili siyo tu kwamba imeamrishwa kusimamisha uhusiano mwema na jamaa, bali imelezwa ya kuwa ni haki yao watendewe wema, na kuwatendea vizuri ndiko kuwatolea haki yao. Neno 'Haki' limetumiwa kwa sababu mara nyingi jamaa wanatakiwa kuwaangalia watoto au wajane, waliofiwa wazazi au waume. Na hao jamaa pia huwa kama wazazi; kwa maana, katika wakati kama huo wanatakiwa kufanya kazi ya wazazi. Hivyo, amesmea Mwenyezi Mungu ya kuwa maadamu jamaa hao wa karibu wametwishwa mzigo wa kuangalia watoto wa jamaa zao wakati wa haja basi ni haki yao hao vile vile kutendewa wema.

Zaidi ya agizo hili kuna maaizo mengine mengi yanayolazimisha kuwatendea wema jamaa. Safari moja, mtu mmoja alimwuliza Mtume[saw]: "Niambie kitendo ambacho nikifanya kitaniingiza peponi." Akamjibu,

kitendo chenyewe ni hiki kwamba umwabudu Mwenyezi Mungu wala usimshirikishe na yeyote, sali na toa zaka, na **watendee wema jamaa zako.**

## Agizo la Kuwatendea Wema Jirani na Wenzi

Zaidi ya jamaa wa karibu wamhusuo mtu kwa damu, kuna namna nyingine vile vile ya watu walio karibu naye wasiomhusu kwa damu. Kwa sababu ya kukaa pamoja naye wanakuwa nao wa karibu. Hivyo, Uislamu haukuwasahau hao vile vile. Juu yao imesewa:

وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنْبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿٣٦﴾

> Yaani, Mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote, na wafanyieni hisani wazazi na pia jamaa za ukoo, na yatima na maskini na jirani ambaye anakaa karibu nanyi; pia jirani aishiye mbali kidogo. Yaani yule jirani ambaye nyumba yake si karibu sana lakini anakaa katika mtaa ule ule mmoja au kijiji kile kile au kijiji kilicho karibu. Na vile vile mtendeeni wema mshiriki wenu katika biashara au afanyaye kazi pamoja nanyi mahali pamoja au aliye pamoja nanyi katika safari, (4:37).

Hayo ndiyo maagizo yaliyotolewa na Uislamu kuhusu jirani na marafiki ya kwamba mmoja wao kwa sababu ya kukaa karibu na nyumba na mwingine kwa kuwa ni

sahibu katika kazi, anaingia katika jamaa wa karibu. Mtume[saw] amesema ya kwamba malaika Jibrili aliniusia mara nyingi sana kuwatendea wema jirani mpaka nikadhani huenda atamfanya jirani kuwa mrithi. Kadhalika, alisema Mtume[saw] kuwahusu masahibu katika safari ya kuwa kama mtu anampanda ngamia basi inampasa kumpandisha mwenziwe pamoja naye kama iko nafasi ya mtu wa pili. Na kama aliye safarini ana chakula kingi kidogo, basi amkaribishe mwenziwe.

Zaidi ya sahibu katika safari, Uislamu umeagiza kuwatendea wema wakaao katika mkutano mmoja. Unasema:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُواْ فِى ٱلْمَجَٰلِسِ فَٱفْسَحُواْ يَفْسَحِ ٱللَّهُ لَكُمْ

> Yaani, Enyi waaminio, mnapokaa mkutanoni na mtu mwingine akija na kuwaombeni kumfanyia nafasi ili akae basi inawapaseni kumfanyia nafasi kwa kukaa karibu zaidi. Mwenyezi Mungu Atawajaalieni ukaribu naye, (58:12 ).

Mtume[saw] ameamuru kuheshimu maoni ya wale ambao mtu anakaa nao. Akasema, kama watu watatu wamekaa mahali pamoja, basi wawili kati yao wasinong'onezane; maana kwa sababu hiyo yule wa tatu ataudhika.

## Wadogo Kuwatendea Wakubwa, na Wakubwa Kuwatendea Wadogo

Zaidi ya maagizo marefu juu ya uhusiano ulioelezwa juu, kuna agizo jingine vile vile lihusulo watu wote. Mtume[saw] amesema:

مَنْ لَمْ يَرْحَمْ صَغِيْرَنَا وَلَمْ يُوَقِّرْ كَبِيْرَنَا فَلَيْسَ مِنَّا

> Yaani, asiyewarehemu wadogo na kuwaheshimu wakubwa, basi hayupo pamoja nasi.

Katika fungu hili fupi lakini lenye maana kamili yamelezwa maungano yote yanayowahusu wadogo na wakubwa.

## Kumtendea Wema Mgeni

Pamoja na kuagiza kuwatendea wema wanaohusika nasi, Uislamu haukumsahau mgeni. Mtume[saw] amesmea;

مَنْ يُؤْمِنُ بِاللهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ فَلْيُكْرِمْ ضَيْفَهُ

Yaani, amwaminiye Mungu na siku ya mwiho yampasa kumheshimu mgeni.

## Uhusiano na Adui

Zaidi ya uhusiano wa urafiki na upendo, mtu anao uhusiano mmoja na adui vile vile. Na huu ndio uhusiano ambao mtu anapokuwa nao, hali yake kujulikana ya kwamba ana jazba kiasi gani ya kuwatendea viumbe vya Mungu. Kwani, mtu

anapokuwa na upendo, basi hulazimika kuwatendea watu wema kwa sababu ya mapenzi yake. Lakini kama hakuna upendo bali upo uadui, basi hapo ndipo ijulikanapo hali ya moyo wa mtu. Basi, ile dini ifundishayo hata kuwahusu maadui maagizo yenye huruma na rehema yasiyo na fujo na shari ndani yake, hiyo ndiyo dini inayostahili kupewa kazi ya kusuluhisha dunia nzima.

Dini mbalimbali zimetoa maagizo tofauti kuwahusu maadui, lakini kwa kufikiria kidogo tu yaweza kujulikana ya kwamba yale mafundisho yaliyotolewa na Uislamu juu ya kuwatendea maadui ndiyo yawezayo kuwa sababu ya kusuluhisha kila zama na kila nchi. Na ndiyo yawezayo kuleta amani na usalama ulimwenguni.

Uislamu unagawanya uadui katika sehemu mbili: Kwanza, uadui wa kidini, pili, wa kidunia. Uadui wa kidini, muradi wake ni ule unaosababishwa na hitilafu za dini; na uadui wa kiduinia ndio ule ambao sababu yake ni ugomvi na uharibifu katika mambo ya kidunia. Kuhusu namna zote mbili za uadui, dini ya Kiislamu imetoa maagizo tofauti. Hivyo, naman zote mbili zitaelezwa mbalimbali.

Kwazna twachukua uadui wa kidunia ili tuone Islam imetoa agizo gani. Lakini, pia ikumbukwe ya kuwa uadui usababishwao na ugomvi au ufisadi katika mambo ya kidunia, Islam imeugawanya tena katika sehemu mbili:

Uadui unaohusu moyo, na uadui unaotokana na vitendo. Kuhusu uadui wa kimoyo agizo la Islam ni kwmba msiujali hata kidogo, wala miswe na bughudha kwa mtu yeyote miongoni mwenu, mpaka imekatazwa pia kuacha kusemezana na mtu kwa sababu ya ugomvi. Bali, amesema Mtume[saw] ya kwamba kuacha kusemezana na mtu zaidi ya siku tatu kumekatazwa. Alisema tena ya kuwa yule anayetangulia kufanya mapatano na mgomvi wake kwa kujiondolea hasira moyoni mwake anastahili rehema ya Mwenyezi Mungu. Ilmuradi, Islam inakataza kabisa uadui wa kimoyo, na inawazuia vikali wafuasi wake wasiuangukie. Kwani, huo ni kama sumu kwa mtu inayoangamiza ndani ka ndani huluka zote njema na matokeo yake yanakuwa fitina zenye hatari ziendeleazo toka kizazi hata kizazi na kuangamiza mataifa.

Hayo ndiyo maagizo unayoleta Uislamu kuhusu ule uadui ukaao moyoni. Ama uadui unaohusu matendo, yaani ule usiokaa moyoni tu bali wadhihrikika kwa kitendo, kwa mfnao mtu mmoja anamwudhi mwingine na kumtaabisha kwa dhuluma, basi kumhusu yeye agizo la Kiislamu ni kwamba hata kwa huyo, mtu asiwe na budhudha moyoni mwake. Kwani bughudha imekatazwa kwa hali yoyote; maana hiyo yaleta fitina na kuharibu khulka. Ama kumlipa adui kwa kitendo cha shari, juu yake kuna maagizo mawili; Kwanza,

sameheni; pili, mwadhibuni. Maagizo haya mawili yanahusu nyakati mbalimbali. Mahali fulani imeagizwa kusamehe na mahali pengine kuadhibu. Maagizo hayo mawili pamoja na mahali pake yamelezwa katika aya hii:

وَجَزٰٓؤُا سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثۡلُهَا ۚ فَمَنۡ عَفَا وَاَصۡلَحَ فَاَجۡرُهٗ عَلَى اللّٰهِ ؕ اِنَّهٗ لَا يُحِبُّ الظّٰلِمِيۡنَ ﴿۴۱﴾

> "Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao; lakini anayesamehe na kusuluhisha, basi ujira waka ni juu ya Mwenyezi Mungu; hila shaka Yeye Hawapendi wadhalimu," (42:41).

Katika aya hii Mwenyezi Mungu amemwagiza mumini njia mbili za kumtendea adui juu ya shari yake. Kwanza, apatiwe adhabu sawa na shari yake; pili, kumsamehe. Na wakati wa kushika njia hii au ile pia umeelezwa. Ikiwa kuna tumaini kuwa kumsamehe adui kutamsuluhisha, basi hapo inapaswa kusamehe, lakini kama kusamehe hakuwezi kumsuluhisha basi apatiwe adhabu. Na maagizo haya, kwa hakika, ni kwa ajili ya watu wa tabia za namna mbili. Twaona kuna watu wa namna mbili. Wa kwanza ni wale ambao makosa yao yakiachiliwa mbali, nao wanasamehewa juu ya wao kufanya shari, huathirika sana mpaka wanajizuia kufanya uadui na wanasikitikia sana yale waliyotenda na wanakuwa marafiki badala ya kuwa maadui. Hii sababu pia imeelezwa na Kurani Tukufu yenyewe, kama ilivyosema:

وَلَا تَسۡتَوِي ٱلۡحَسَنَةُ وَلَا ٱلسَّيِّئَةُۚ ٱدۡفَعۡ بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُ فَإِذَا ٱلَّذِي بَيۡنَكَ وَبَيۡنَهُۥ عَدَٰوَةٞ كَأَنَّهُۥ وَلِيٌّ حَمِيمٞ ۝٣٥

> "Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Zuia ubaya kwa yaliyo mema zaidi, na mara yule ambaye baina yako na yeye pana uadui atakuwa kama rafiki sana", (41:35).

Yajulikana kwa aya hii, Mwenyezi Mungu ameweka hekima gani katika msamaha na shabaha yake ni nini. Basi, kama ilivyo dhahiri katika aya ile ya kwanza, inapasa kusamehe hapo tu msamaha unaposuluhisha. Na ambapo msamaha hausuluhishi, bali mtu mwovu anazidi katika ubaya, basi hapo inatakiwa kumwadhibu. Kwani, wakati huo kumsamehe mtu huyo ni kumdhulumu yeye pamoja na wanadamu wengine. Maana, kumsamehe yule azidiye katika shari kwa sababu ya msamaha, na hajinyoshi bila kuadhibiwa, matokeo yake yatakuwa kwamba atajasiri zaidi juu ya shari na atawadhulumu watu wengine pia. Na atakapogombana kidogo tu na mtu basi atajaribu kumwangamiza kabisa, na hivyo fitina itazidi duniani. Na sababu ya fitina hii yote kuenea atakuwa ni yule mtu aliyemwacha bila adhabu mtu mwenye shari awaudhiye wengine na kuwadhulumu — na akamsamehe juu ya kwisha kupeleleza kwamba hajinyoshi kwa kusamehewa.

Hapa, huenda itapita fikira mioyoni mwa watu ya kuwa yawezaje kujulikana kuwa mtu ambaye nimekabiliana

naye atajisuluhisha kwa kuadhibiwa au kusamehewa? Jibu lake ni kwamba jambo hili litajulikana baada ya majaribio. Kama ikionekana baada ya kujaribu mara mbili tatu kuwa mtu fulani hajitengenezi kwa kuachilwa na kusamehewa, basi kumwadhibu kutakuwa bora. Na kama inajulikana kwa majaribio kwamba anaacha uadui na shari kwa kusamehewa, basi asamehewe. Na hayo ndiyo maagizo ya katikati ya uadilifu. Na kama yapo maagizo ghairi ya hayo, basi lazima hayo yawe kwa muda mfupi tu. Kwa mfano, Wayahudi, kwa sababu ya kutawaliwa kwa muda mrefu, waliamrishwa kwa mkazo sana kuadhibu na kujilipiza kisasi, ili wapate idili na nguvu. Na matokeo yake yalikuwa kwamba Wana wa Israeli wa zama za Musa[as] wakaepuka unyonge wao katika muda mfupi tu. Waila hali yao ilikuwa kwamba Firauni majeshi yake yalipowazunguka basi juu ya dhuluma za Firauni, walikuwapo wengi walioridhika kurudi. Hali hii hupatikana kaumu inapokuwa na woga kupita kiasi. Waila kwa kuchukizwa na mdhalimu na msumbufu hata wanyama wasio wakali wanakuwa tayari kupambana, ilihali wanakuwa si kitu mbele ya adui wao. Basi, kuwa tayari kwa baadhi ya makabila ya Wana wa Israeli kurudi, na kisha kuogopa kwao katika kila hatua, kunaonyesha ya kuwa wakati huo walikuwa watu duni sana katika uhodari na ushujaa. Basi ilibidi kutilia mkazo jambo hili ya kwamba lazima wajilipize kisasi, ili

kuwainua na kuwaendeleza mbele. Na wakati huo agizo hili tu lilikuwa sawa na hali yao ya kuwa:

> "Wala jicho lako lisiwe na huruma; uzima kwa uzima, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu" (Kumbukumbu, 19:21).

Lakini, zama ndefu zilipokuwa zimepita na Wana wa Israeli walipotenda sawa na sheria hii kizazi baada ya kizazi, wakawa na tabia ya ukatili, na nyoyo zao zikawa ngumu. Basi, ili kuondolea mbali tabia hii ikatangazwa na Yesu ya kwamba:

> "Mmesikia kwamba imenenwa, Jicho kwa jicha, na jino kwa jino; lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili. Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia. Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili. Akuombaye, mpe, naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo.
>
> "Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na Umchukie adui yako, lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi", (Mathayo 5:38-44).

Wale waliotii tangazo hilo, wakatenda sawa nalo na wakatupilia mbali ukatili uliokuwa umekwisha patikana mioyoni mwa Wana wa Israeli. Na pole pole kundi moja

likapatikana la watu waliokuwa wenye mapenzi na mahaba badala ya kugombana na kubishana. Lakini, je, fundisho hili liliweza kufaa siku zote na kwa nchi zote? Je, amani ingaliweza kustawi duniani kwa fundisho hili, na ingaliwezekana kumsuluhisha binadamu? Bila shaka fundisho hili lilileta matokeo mema na mazuri sana katika wakati wake, lakini, liliweza kuenezwa katika watu hao hao ambao kwa sababu ya kutenda sawa na mafundisho ya Musa[as] walikuwa wamepita mipaka; waila ilikuwa haiwezekani kwa dunia nzima kulitekeleza, si katika wakati ule wala baadaye. Ndipo ilibidi kufika duniani maagizo kutoka kwa Mwenyezi Mungu yenye kuwa na pande zote hizo mbili, na yenye kumwongoza binadamu sawa na hali. Basi, ikaja Kurani Tukufu. Na kama ilivyokwisha somwa mbele yenu sasa hivi, Kurani Tukufu, upande mmoja, iliweka mbele za watu Sheria ya Musa ya kwamba mwadhibuni mwenye shari na mwovu sawa na uovu wake, na upande mwingine ikaleta maagizo ya Yesu vile vile ya kuwa umtendee wema sana mwovu kwa kulipa uovu wake. Na zaidi ya mafundisho haya mawili ikaeleza kuwa ikiwa kuadhibu kwaleta islahi, adhibuni; na kusamehe kuletapo islahi, sameheni. Ilmuradi, katika njia hizi mbili yoyote iliyo sawa na hali ya mtu huyo, tumia ile tu, ili amani hasa ipatikane duniani, na dhuluma na uadui vifutike duniani. Hayo ndiyo maagizo ya katikati yawezayo kufaa kila nchi. Na mtu akifikiria kidogo tu anaweza kujua ya kuwa hakuna

fundisho, ghairi ya hilo, lifaalo kuenezwa katika dunia nzima, na ambalo kwa kulishika hatari ya binadamu kuelekea upande mmoja tu iweze kutoweka kabisa. Tunaweza kudai ya kwamba maagizo makamilifu kama hayo hayamo ndani ya dini nyingine yoyote. Na kama yapo, basi inawalazimu wafuasi wa dini hiyo watuonyeshe hayo pamoja na masharti yake yote kutoka katika vitabu vyao vva kidini.

Kuna dini za namna tatu tu duniani. Zile ziagizazo kufanya uovu ili kulipa uovu; au zile zisemazo kwamba ufanye wema kulipa uovu; au zile ambazo bila kutaja sharti yoyote zinasema kwamba usamehe na pia uadhibu. Lakini, hamtakuta dini yoyote, isipokuwa Islam, imwambiayo binadamu kuadhibu wakati gani na kusamehe wakati gani. Na mpaka dini ieleze sababu vile vile fundisho lake haliwezi kuhesabiwa ni kamilifu.

## Uadui wa Kidini

Baada ya kueleza haya, sasa twawajia maadui wa kidini ili tujue imeagizwa nini kwa kuwatendea hao. lkumbukwe, basi, ya kwamba Islam inaona hitilafu ya dini na uadui wa kidini kuwa mambo mawili mbalimbali. Uislamu hautufundishi ya kuwa wanaohitilafiana nasi katika dini tuwafikirie na kuwatendea kama maadui. Bali, Uislamu unatuagiza kwamba: Watendeeni wema wafuasi wa dini zote zile, wala msifikirie hitilafu ya dini kuwa ni uadui. Na wale

wasio na uadui kwenu wala hawawadhulumuni kwa sababu ya hitilafu za dini, mwafanyie hisani na kuwatendea kwa murua na wema na adili. Lakini wale ambao hawavumilii itikadi yoyote iliyo kinyume na itikadi yao, basi jitengeni nao kabisa. Kwani, ni kinyume na ghera ya kwamba mfanye urafiki na mtu apendaye kufuta dini yenu kwa upanga na anamtukana Mwenyezi Mungu na Kitabu chake. Mwenyezi Mungu anasema katika Kurani Tukufu:

لَا يَنْهٰىكُمُ اللّٰهُ عَنِ الَّذِيْنَ لَمْ يُقَاتِلُوْكُمْ فِي الدِّيْنِ وَلَمْ يُخْرِجُوْكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ اَنْ تَبَرُّوْهُمْ وَتُقْسِطُوْٓا اِلَيْهِمْ ۭ
اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِيْنَ ۝ اِنَّمَا يَنْهٰىكُمُ اللّٰهُ عَنِ الَّذِيْنَ قٰتَلُوْكُمْ فِي الدِّيْنِ وَاَخْرَجُوْكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ وَظٰهَرُوْا عَلٰٓي
اِخْرَاجِكُمْ اَنْ تَوَلَّوْهُمْ ۚ وَمَنْ يَّتَوَلَّهُمْ فَاُولٰۗىِٕكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ۝

> Yaani, Mwenyezi Mungu Hawakatazeni wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakuwafukuzeni katika nyumba zenu ya kwamba mwafanyie hisani na adili. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu. Mwenyezi Mungu Anawakatazeni wale tu ambao hupigana nanyi katika dini na huwafukuzeni katika nyumba zenu, na wanasaidia juu ya kuwafukuzeni ya kwamba msipendane nao. Na wafanyao urafiki nao, basi hao ndio wadhalimu. (60:9-10)

Kwani, mtu kama huyo anakuwa sababu ya kumhimiza adui afanye kitendo kiovu, na kwa sababu ya kitendo chake huenda adui akafikiria kumbe juu ya mimi kutukana dini yake yeye hukutana nami kwa

shauku, basi haikosi ataathirika nami. Na hutukia mara nyingi ya kwamba mtu asiyekuwa na ghera huathirika pole pole kwa mawazo ya wengine. Basi, ili kuhifadhi dini na kuiweka hai huluka njema sana kama ghera, ilibidi kutoa amri kama hii ya kuwa mtu anayekuwa tayari kupigana juu ya mambo ya dini na anapatwa na hasira kali asikiapo juu ya itikadi iliyo kinyume na itikadi yake, hata kwamba hawezi kuangalia masharti madogo madogo ya ubinadmau, awezaje kustahili kufanywa rafiki? Na juu ya hayo yote ikiwa mtu anampenda yeye, basi bila shaka moyo wake hauna ghera. Ndio kusema katika fundisho hili vile vile Uislamu umeshika njia ya katikati kwa kujiepusha na pande zote mbili za kupita kiasi na kupuguza. Upande mmoja umesimamisha mapenzi na huruma, na upande mwingine umebakiza hai ghera iliyo huluka njema sana — ambayo bila kuwa nayo mwanadamu anakuwa kama mnyama — ili kwamba mfuasi wake asipate kuelekea upande mmoja tu. Hayo ndiyo maagizo ambayo mfano wake haziwezi kuuleta dini zisizohalalisha uhusiano wa namna yoyote na dini nyingine, wala zile ziagizazo kuwa na upendo tu juu ya uadui mkali kabisa wa kidini. Maana, hizo zavunja tabia ya asili ya kibinadamu, na matokeo yake hayawezi kuwa mema.

## Kuwatendea Wanadamu wote kwa Jumla

Sasa, naeleza maagizo ya Islam juu ya wale wasiomhusu mtu dhati yake. Wa kwanza kabisa katika aina hii ya watu ni mayatima na maskini. Ingawaje yatima na maskini anaweza kuwa jamaa vile vile, lakini kwa kuwa Uislamu haukuweka sharti kwamba awe miongoni mwa nani, hivyo nawaweka hao chini ya kichwa cha maneno 'Watu kwa jumla'. Kwani, mayatima na maskini anaowashughulikia mtu huwa mara nyingi si jamaa zake. Kuhusu nama hizi mbili (yatima na maskini) Uislamu umeagiza maagizo mengi mno yasiyoweza kuelezwa hapa, maana madhumuni yamekwisha kuwa marefu sana. Wakati huu, inatosha tu kueleza ya kuwa dini ya Kiislamu imetilia mkazo sana kuwatendea wema mayatima na maskini. Kuhusu jambo hili sehemu ya maelezo imekwisha elezwa hapo juu. Hapa itatosha tu kueleza kuwa kutokuwatendea wema mayatima, Kurani Tukufu yasema, ni miongoni mwa matendo ambayo matokeo yake huwa udhalilifu. Basi, yasema kuwa waadhibishwapo baadhi ya watu, husema Mungu ametutendea hivi, lakini Mwenyezi Mungu anasema juu yao:

كَلَّا بَل لَّا تُكْرِمُونَ الْيَتِيمَ ﴿١٨﴾

Sivyo msemavyo. Bali ninyi mlikuwa hamwaheshimu mayatima; bali hata hamkuwaangalia mlipowaona katika hali mbaya, (89:18).

Kuhusu maskini anasema ya kuwa kutowatendea wema ni katika vitendo vimtupavyo mtu motoni. Anasema juu ya baadhi ya waendao motoni:

وَلَا يَحُضُّ عَلَىٰ طَعَامِ الْمِسْكِينِ ﴿٣٥﴾ فَلَيْسَ لَهُ الْيَوْمَ هَاهُنَا حَمِيمٌ ﴿٣٦﴾

> Wala hakuhimiza juu ya kulisha maskini. Basi leo hapa hana rafiki mpenzi, (69:35-36).

Yaani, kwa kuwa hawakuhimiza juu ya kuwaangalia maskini, basi Mwenyezi Mungu hakuwasaidia, waila angewaokoa katika adhabu.

## Maagizo Kuhusu Wanadamu Wengine Ghairi ya Mayatima na Maskini

Miongoni mwa maagizo yaliyotolewa na Uislamu kuhusu wanadamu wote kwa jumla, mojawapo ni hili ya kwamba ikiwa mtu anapata kujua kwa ghafula uovu wa mtu mwingine, basi inampasa kuusitiri. Mtume[saw] amesema:

لَا يَسْتُرُ عَبْدٌ فِي الدُّنْيَا إِلَّا سَتَرَهُ اللهُ فِي يَوْمِ الْقِيَامَةِ

> Yaani, mtu anayesitiri aibu ya mtu mwingine, basi Mwenyezi Mungu atamsitiria aibu yake siku ya Kiyama.

Pia, imeagizwa ya kuwa si halali kwa Mwislamu kuchukua riba kwa mtu yeyote. Bali, kama yupo mwenye haja, basi amsaidie iwezekanavyo au amkopeshe tu. Maana, riba ni dhuluma ambayo mtu anamfanyia

mwingine. Ndugu mmoja anapokuwa na haja, huyu anataka kumnyang'anya ndugu yake mali zaidi.

Katika maagizo haya kuna hili pia ya kuwa mtu haruhusiwi kwenda haja katika maji yaliyotulia. Kwani, matokeo yake yatakuwa ya kwamba kama watu watayatumia kwa haja fulani, watapata madhara kwa kuwa yamenajisika. Tena, miongoni mwa mafundisho uliyotoa Uislamu kwa manufaa ya wanadamu wote kwa jumla ni hili ya kuwa mtu hana ruhusa ya kujisaidia chini ya mti wenye kivuli, njiani, au mahali pa kuteka maji. Maana kitawadhuru wasafiri waliochoka, watumiao barabra na watu wenye kiu.

Zaidi ya hayo kuna agizo lingine pia la Islam ya kwamba mtu asifike msikitini baada ya kula kitu chochote chenye harufu mbaya kimfanyacho kupiga piga mbweu mbaya au hukifanya kinywa kinuke vibaya. Hili pia ni agizo ambalo lahusu yale mafundisho ambayo shabaha yake ni kuwahurumia wanadamu kwa jumla. Kwani, kwa kufanya hivyo watu wengi huudhika. Msikiti umetajwa kwa sababu Waislamu wanakutanika misikitini, waila amri hii inahusu mahali popote pale. Na hii amri ni muhimu sana kiasi ambacho siku hizi imeibidi idara ya Relwe kutengeneza sheria ya kuwa mtu yeyote asivute sigara katika gari la moshi, kwa kuwa masingasinga huudhika kwayo. Kama ikitendwa sawa na agizo la Kiislamu, hakuna haja tena ya kutengeneza sheria nyingine zaidi. Na athari ambayo dini inaleta juu ya matendo ya binadmau, haiwezi kanuni ya nchi kuileta.

Tena, miongoni mwa maagizo haya kuna jambo hili vile vile ya kuwa mahali unapoenea ugonjwa wa kuambukiza, watu hawaruhusiwi kupahama na kuikimbilia miji mingine. Kwa maana, matokeo yake yatakuwa kwamba ugonjwa huo utaenea mahali hapo vile vile palipokuwa na salama. Uzuri wa amri hii India imekwisha ujua sana hivi karibuni. Maana tauni kuenea sana kulisababishwa na kutofanya sawa na amri hii. Tauni ilipoenea mahali fulani, watu walikimbilia miji mingine, basi nayo ikaenea mahali pale vile vile. Kama nchi ya India ingekuwa ya Waislamu, nao wangefanya sawa na agizo hilo, mnaweza, basi, kuelewa ya kwamba ugonjwa ungezuilika namna gani! Sio muradi wa agizo hili ya kuwa imekatazwa hata kuondoka mji na kukaa nje yake, bali imekwisha thibitika katika desturi ya masahaba kwamba wakati wa tauni na magonjwa mengine kama hiyo inafaa kutawanyika misituni. Muradi wa agizo hili ni huu tu ya kwamba kuondoka mji ulimoenea ugonjwa na kwenda mahali palipo salama hakufai.

Kadhalika kwa kuwahurumia wanadamu Dini ya Kiislamu imeamuru vile vile ya kuwa ikiwa mtu anaona kitu chenye kudhuru njiani yampasa akiondoe. Kwa mfano, liko jiwe barabarani au tawi lenye miiba liwezalo kuwa sababu ya wapitao kuanguka au kujeruhiwa, basi liondolewe mbali. Na Mtume[saw] amehesabu tendo hilo katika sadaka. Na fundisho hili ndilo ambalo haiwezi dini nyingine kuleta mfano wake.

## Kuwatendea Wema Wanyama

Uislamu ulipoagiza juu ya kuwatendea wema wanadamu, ndipo ulipoagiza pia juu ya kuwatendea wema wanyama. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Kurani Tukufu:

وَفِيٓ أَمۡوَٰلِهِمۡ حَقّٞ لِّلسَّآئِلِ وَٱلۡمَحۡرُومِ ٢٠

Yaani, Mwislamu ni yule ambaye katika mali zake imo haki ya wale wawezao kuomba — yaani wanadamu — na ya wale wasioweza kuomba, yaani wanyama, (51:20).

Yaani, ni juu ya Mwislamu kuwashirikisha wanadamu wenye haja na wanyama katika mali yake. Kadhalika, imesimuliwa katika Hadithi ya Mtume[saw] ya kuwa imekatazwa vikali kumwudhi mnyama, hata kwamba Mtume[saw] amemlaani yule amfungaye mnyama kisha kumlenga. Na Mtume[saw] tu ndiye aliyekataza kuwatia wanyama alama ya moto usoni, kwani uso ni sehemu laini; basi alikataza kutia alama usoni. Naye aliamuru kutia alama katika sehemu ya juu ya paja la nyuma. Nayo ndiyo desturi ipatikanayo duniani siku hizi. Kadhalika, imesimuliwa na Mtume[saw] ya kwamba mwanamke mmoja alimfunga paka, na paka yule alikufa kwa njaa na kiu, basi Mwenyezi Mungu akamtia motoni. Yaani, kwa sababu ya ukatili huu, mwanamke huyo aliangukia matendo yaliyomwingiza motoni.

Basi, Uislamu umeamrisha kuwatendea wema wanyama na kukataza kuwafanyia ukatili na kuwaudhi bila sababu. Hivyo, Uislamu umekamilisha maagizo yake kila

upande. Uislamu haukukazania jambo moja tu, bali umetoa maagizo yenye uadilifu na usawa kuhusu mahitaji yote ya binadamu na kila sehemu ya maisha yake. Maagizo hayo mtu akiyafuata anaweza kufurahi na kupata raha katika dunia hii na Akhera pia.

Hivyo, ni dini ya Kiislamu tu ambayo inaweza kufuatwa na watu wote. Dini hii ndiyo ya pekee ambayo watu wa kila namna na kila tabia wanaweza kutenda sawa na mafundisho yake. Wala kutenda sawa nayo hakuleti uharibifu wowote, bali yaweza kushikwa nyakati zote, nayo ndiyo njia ya kumwokoa mwanadamu. Mambo yote mazuri yapatikanayo katika dini mbalimbali, hayo yote yamekusanyika katika Uislamu. Nayo imechukua ndani yake maagizo yote yenye manufaa na baraka. Na kwa kuwa Islam ndiyo dini ya mwisho kuletwa na Mwenyezi Mungu, basi mtu anaweza kuokoka kwa kufuata hiyo tu peke yake. Dini ya Islam ndiyo ambayo pekee inamwunganisha mwanadamu na Mwenyezi Mungu katika dunia hii na inatoa matunda yake daima. Ndio maana, wale walioifuata dini hii, waliendelea kumfikia Mwenyezi Mungu katika kila zama na wakati. Na katika zama hizi pia, mti huu umetoa matunda yake matamu. Mwenyezi Mungu amekwisha mtuma mfuasi mmoja wa dini hii, Seyidna Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] na kamfanya awe Masihi aliyeahidiwa na Mahdi aliyebarikiwa kwa kutengeneza hali ya watu wa siku hizi.

Basi, Enye mtafutao ukwelii na mpendao haki, simameni wima na njooni kwenye chemchem hii safi

baada ya kukata minyoror yote na kuvuka vizuizi vyote. Furaha, raha na utulivu unaotaka tabia yenu ya asili haupatikani katika wakati huu ila katika Uislamu. Na dini hii tu ndiyo inayoweza kuwafikisheni kwenye darja la juu la maendeleo ya kiroho. Hata mnaweza kumpata Mwenyezi Mungu katika hii hii dunia na kufika kwenye daraja ya yakini baada ya kuondoka katika shaka na wasiwasi wote.

Mimi,<br>
Mahmood Ahmad,<br>
wa Qadian.